# Nipashe

Jumanne Mei 24, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580955

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

LIKE & FOLLOW US



BREAKING NEWS

CHEZA JACKPOT

TZS 222,883,040

KWA 1000/- TU!

SportPesa.CO.TZ | PIGA *150*87#




**Mwingine** auawa kwa kupigwa risasi mgodini

UKURASA 7



**IBRAHIMOVIC: NITAENDELEA KUCHEZA MSIMU MWINGINE**

UKURASA 21

# CHADEMA yaomba usalama kina Lissu

UKURASA 2

## YALIYOMO

UKURASA WA 3

### ACT: MCHAKATO KATIBA MPYA UANZE OKTOBA

CHAMA cha ACT-Wazalendo kimetoa mapendekezo 10 kwa Kikosi Kazi cha Rais Samia Suluhu Hassan, ikiwamo kuitaka serikali kuanza...



Mbunge wa Mbulu Vijijini, Flatei Massay, akipiga sarakasi ndani ya ukumbi wa Bunge alipochangia bungeni jana hoja ya makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kwa mwaka 2022/23, ili kufikisha ujumbe kwa serikali kuhusu hoja yake. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Mbunge alivyopiga sarakasi

UKURASA 3




Waziri wa Ujenzi, Prof. Makame Mbarawa, akiwasilisha bungeni jana hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi ya wizara yake kwa mwaka 2022/2023, jijini Dodoma. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mikakati Ujenzi 'usipime', Sh. trilioni 3.8 uwanjani

UK. 2


**MICHEZO** YANGA BADO POINTI 3 BINGWA UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6




Makamu wa Rais, Dk. Philip Isdor Mpango, akizungumza katika mkutano wa Jukwaa la Uchumi Duniani unaofanyika Davos nchini Uswisi wakati wa mada ya kukabiliana na changamoto ya ukosefu wa chakula duniani jana. **PICHA: OFISI YA MAKAMU WA RAIS**

# CHADEMA yaomba usalama kina Lissu

**Na Mwandishi Wetu**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kimewasilisha kwa serikali hoja kuu mbili za kufanyia kazi ambazo ni kushughulikia madhara yaliyotokana na ukiukwaji wa haki pamoja na kurejeshwa na kukamilishwa kwa mchakato wa Katiba Mpya.

Katika hoja yake ya kwanza inayohusu haki, chama hicho kimeiomba serikali kuwahakikishia usalama viongozi na aliowaita wakimbizi wa kisiasa.

Viongozi wa chama hicho wanaoishi nje ya nchi kwa sasa kutokana na kile wanachodai tishio la usalama wao ni pamoja na Makamu Mwenyekiti, Tundu Lissu na aliyekuwa Mbunge wa Arusha Mjini, Godbless Lema.

Katibu Mkuu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), John Mnyika, jana alipozungumza na waandishi wa habari, alibainisha kuanza kwa mazungumzo kati ya ujumbe wa chama hicho ulioongozwa na Mwenyekiti, Freeman Mbowe na upande wa serikali ulioongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan.

"Katika kikao chetu na viongozi wa CCM na serikali, tulitaka hakikisho la usalama kwa viongozi na wakimbizi wengine wa kisiasa walioko nje ya nchi.

"Vilevile, tulitaka kuondolewa bungeni kwa waliokuwa wanachama 19 wa CHADEMA na kushughulikia masuala yaliyowakumba viongozi kutokana na ukandamizwaji wa demokrasia," Mnyika alisema.

Aliendelea: "Kuhusu katiba mpya, tunaamini ni nyenzo kuu ya kulipeleka taifa letu mbele na kufungua ukurasa mpya wa kimfumo na kitaasisi. Katika nchi yetu tumepeleka upande wa serikali mapendekezo yetu juu ya namna ya kung'amua mchakato wa katiba ulipokwamia."

Alisema katika hilo rai na mapendekezo yao wameelekeza katika kuwa na ratiba na taratibu zitakazowezesha Katiba Mpya kukamilika kabla ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025.

Kuhusu madhara yaliyotokana na ukiukwaji wa haki, Mnyika alisema katika mazungumzo yao na upande wa serikali, waliwasilisha mapendekezo 10 ikiwamo kuundwa kwa tume ya ukweli na upatanishi na kushughulikiwa kwa madhara yatokanayo na Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa mwaka 2019 na Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020.

"Jambo lingine ni kufutwa kesi zenye mwelekeo wa kisiasa na kuachiwa kwa wafungwa wa kisiasa. Lingine ni kufutwa au kurekebishwa kwa sheria kandamizi katika nchi yetu. Jambo lingine ni kushughulikia masuala yanayohusu viongozi wa chama na watu walioshambuliwa, kupotea au kuuawa kwa sababu za kisiasa," alisema.

Mnyika ailisema huo ni mwanzo tu wa mazungumzo na hatua nyingine zinafuata na kuwataka wanachama wa chama hicho kuwa watulivu katika hatua hizo zilizoanza kwa kuwa mchakato wa maridhiano na wa muda mrefu unafanyika kwa hatua.

Katibu Mkuu huyo alisisitiza msimamo wa kutoshiriki kutoa maoni katika kikosi kazi kilichoundwa na Rais Samia na kusema kwa taarifa iliyotolewa na Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa kuwa chama hicho kitatoa maoni mbele ya kikosi kazi leo si ya kweli.

"Ninaomba umma na wanahabari mfahamu kuwa CHADEMA haitakwenda kesho (leo) 24 Mei kutoa maoni mbele ya kikosi kazi. Msimamo wetu kuhusu mchakato unaoendelea wa kikosi kazi ni ule ule haujabadilika," alisema Mnyika.

**KAULI YA CCM**

Katibu wa Halmashauri Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Itikadi na Uenezi, Shaka Hamdu Shaka, alisema jana jijini Dodoma kuwa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya chama hicho iliyoketi juzi jijini Dodoma, mbali na kupokea na kujadili mambo mbalimbali, ilimpongeza Rais Samia kwa kuwa mstari wa mbele kutafuta maridhiano na viongozi wa kisiasa nchini ili kusaidia uwapo wa haki, amani na umoja wa kitaifa.

"Kamati Kuu imempongeza mwenyekiti wake kwa kuendelea kushiriki majadiliano ya kupata maridhiano na makundi mbalimbali ya kisiasa wakiwamo viongozi wakuu wa vyama, akiwamo (Prof. Ibrahim) Lipumba na hivi karibuni Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe.

"Maridhiano ndiyo njia pekee ya kuendeleza amani, haki na umoja wa kitaifa ambao waasisi wetu walituachia, hivyo Kamati Kuu inampongeza sana Rais Samia kwa kuendeleza jitihada za kutafuta maridhiano nchini," alisema.

Shaka alisema vikao hivyo vya maridhiano ni njia ya kutafuta mwafaka wa pamoja na CCM ipo tayari kuendelea na mijadala ya kuimarisha demokrasia nchini.

Aliwataka Watanzania wote bila kujali itikadi za vyama vyao, kumuunga mkono Rais Samia katika jitihada hizo za kutafuta maridhiano na umoja wa kitaifa.

Rais Samia hivi karibuni alishiriki ufunguzi wa mkutano wa haki, amani na maridhiano ulioandaliwa na Kituo cha Demokrasia nchini (TCD) ambao pamoja na mambo mengine, aliagiza kutolewa maoni ya namna bora ya vyama vya siasa kuendesha mikutano ya hadhara.

Pia, aliagiza kukusanywa kwa maoni yatakayosaidia kufanya mabadiliko ya sheria ya vyama vya siasa na ile ya uchaguzi ambazo zimekuwa zikilalamikiwa na vyama vya siasa.

***Imeandikwa na Jenifer Gilla (DAR) na Paul Mabeja (DODOMA)**

# Mikakati Ujenzi 'usipime', Sh. trilioni 3.8 uwanjani

**Na Romana Mallya,** DODOMA

WAZIRI wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, ameliomba Bunge kuidhinisha Sh. trilioni 3.8 ili kutekeleza majukumu ya wizara hiyo kwa mwaka ujao wa fedha, yakijumuisha ujenzi wa miradi ya barabara, madaraja, vivuko na viwanja vya ndege.

Mbali na miradi hiyo, wizara hiyo pia imeomba kuidhinishiwa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mikubwa ikiwamo ya daraja refu zaidi Afrika Mashariki la Kigongo-Busisi na kulipa madeni ya makandarasi.

Akiwasilisha bungeni jijini hapo jana hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hiyo ya mwaka wa fedha 2022/23, Prof. Mbarawa, alisema watahakikisha wanaongeza ushiriki wa wanawake katika ujenzi kwa kuwapa kipaumbele makandarasi wanawake.

Waziri huyo aliitaja miradi itakayotekelezwa katika sekta ya ujenzi mwaka ujao wa fedha inajumuisha ujenzi na ukarabati wa vivuko na maegesho ya vivuko, Sh. bilioni 13.123 zikitengwa.

"Jumla ya Sh. bilioni 2.585 zimetengwa kwa ajili ya mradi wa ujenzi wa maegesho ya vivuko. Kazi zitakazofanyika ni pamoja na upanuzi wa jengo la abiria katika kivuko cha Magogoni – Kigamboni kwa upande wa Kigamboni; ujenzi wa maegesho mapya ya vivuko vya Kayenze - Kanyinya, Muleba – Ikuza, Ijinga - Kahangala (Magu) na Bwiro - Bukondo (Ukerewe) pamoja na kuboresha mfumo wa tiketi za kielektroniki kwenye vivuko vitano (Magogoni-Kigamboni, Kigongo-Busisi, Kisorya-Rugezi, Pangani-Bweni na Ilagala-Kajeje)," alisema.

Waziri huyo alisema Sh. bilioni 59.817 zimetengwa kwa ajili ya mradi wa ujenzi na ukarabati wa nyumba na majengo ya serikali, ukiwamo mradi wa ujenzi wa nyumba za viongozi wa serikali uliotengewa Sh. bilioni 8.015 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba nyingine 20 za viongozi Dodoma pamoja na kuendelea na ujenzi wa nyumba tano za majaji katika mikoa ya Kilimanjaro, Mtwara, Shinyanga, Kagera na Tabora.

**BARABARA, MADARAJA**

Prof. Mbarawa alizitaja barabara zitakazojengwa kuwa ni pamoja na Soni-Bumbuli-Dindira-Korogwe (Km 74), Mtwara-Newala-Masasi (Km 210), Mnivata-Tandahimba–NewalA-Masasi (Km 160) na Nachingwea-Liwale (Km 130).

Kwa madaraja, Prof. Mbarawa alisema Daraja jipya la Wami limetengewa Sh. bilioni mbili ili kuendelea na ujenzi katika barabara ya Chalinze-Segera na ile ya Njombe-Makete Isyonje (Km 157.4).

Waziri huyo barabara za kuelekea katika vituo vya Reli ya Kisasa (SGR) zenye urefu wa Km 87.6 zimetengewa Sh. bilioni 15.806.

**MADENI, BARABARA ZA JUU**

Alisema Sh. bilioni 13 zimetengwa kwa ajili ya kulipa madeni ya makandarasi na washauri ujenzi wa madaraja ya Magufuli (Morogoro), Ruhuhu (Ruvuma), Mara (Mara), Magara (Manyara), Lukuledi (Lindi), Msingi (Singida) na Kiyegeya (Morogoro).

Prof. Mbarawa alisema wamepanga kuyaboresha makutano ya KAMATA, Magomeni, Mwenge, Tabata/ Mandela, Morocco, Buguruni, Mbezi Mwisho, Fire na yale ya Kinondoni/Ali Hassan na Selander.

Alisema miundombinu ya mabasi yaendayo haraka (BRT) phase I-V (Km 69.8) imetengewa Sh. bilioni 1.065 (fedha za ndani) na Sh. bilioni 48.247 (fedha za nje) zimetengwa kwa ajili ya miundombinu ya awamu ya pili.

"Miradi ya miundombinu ya viwanja vya ndege zimetengwa Sh. bilioni 86.102. Mfuko wa barabara fedha zilizotengwa ni Sh. bilioni 599.756 ili kutengeneza na kukarabati barabara kuu za mikoa," alibainisha.

**USHIRIKI WANAWAKE**

Prof. Mbarawa alisema wizara imepanga kuendelea kutoa mafunzo kwa makandarasi wanawake ya namna ya kuomba zabuni na namna ya kujaza zabuni kwa ufanisi.

Alisema Wakala wa Barabara (TANROADS) umepanga kujenga barabara kuu yenye urefu wa kilometa 470 kwa kiwango cha lami na ukarabati wa kilometa 33 kwa kiwango cha lami katika barabara kuu, ujenzi wa madaraja 10 na ukarabati wa daraja moja, na kufanya upembuzi yakinifu wa makini madaraja sita.

Alisema Bodi ya Usajili wa Wahandisi imepanga kusajili wahandisi 3,200, bodi ya uwasijili wa wabunifu majengo na wakadiriaji wa majengo kusajili wataalamu 125 na ya makandarasi itasajili 960.

"Mamlaka ya Reli Tanzania-Zambia (TAZARA) imetengewa Sh. bilioni 22.2 vyanzo vya mapato ya ndani na Sh. bilioni 13.19 kutoka mfuko mkuu wa serikali," alisema.

## HABARI KITAIFA




Katibu Mkuu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), John Nyika, akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# ACT: Mchakato Katiba Mpya uanze Oktoba

**Na Maulid Mmbaga**

CHAMA cha ACT-Wazalendo kimetoa mapendekezo 10 kwa Kikosi Kazi cha Rais Samia Suluhu Hassan, ikiwamo kuitaka serikali kuanza mchakato wa kupata Katiba Mpya mwezi Oktoba mwaka huu hadi Agosti 2024 chini ya rasimu ya Jaji mstaafu Joseph Warioba.

Mapendekezo hayo yaliwasilishwa jana jijini Dar es Salaam na Makamu Mwenyekiti wa chama hicho Tanzania Bara, Dorothy Semu. Kiongozi huyo alifuatana na wajumbe wengine wa chama hicho ambao ni pamoja na Naibu Katibu Mkuu Bara, Joran Bashange, Katibu wa Habari, Uenezi na Uhusiano na Umma, Salim Bimani, na Naibu Katibu wa Haki za Binadamu na Makundi Maalum, Pavu Abdallah.

Semu alisema chama hicho kinapendekeza kupitiwa upya na kufanya marekebisho ya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba (Constitutional Review Act) na Sheria ya Kura ya Maoni (Referendum Act) ili kukidhi matakwa ya sasa na kuamua mchakato wa kupata Katiba Mpya uendelezwe kuanzia hatua ipi, pia kutambua maeneo yaliyosababisha mkwamo katika mchakato wa 2011-2014.

"Tunapendekeza kujengwa mwafaka wa kitaifa kuhusiana na maeneo muhimu yanayogusa mfumo wa kikatiba wa Jamhuri ya Muungano ambayo yamekuwa ndiyo chanzo na sababu ya mivutano katika maudhui ya Katiba Mpya.

"Maeneo hayo ni pamoja na Muungano na muundo wake; madaraka ya Rais; mgawanyo wa madaraka kati ya Bunge, Serikali, Mahakama; mfumo wa uchaguzi na uendeshaji wake na Katiba Mpya kufikishwa kwa wananchi kwa ajili ya kupigiwa kura ya maoni," alisema Semu.

Mapendekezo mengine yalitolewa na chama hicho kwenye maeneo yaliyoainishwa na kikosi kazi hicho ambayo ni: Mikutano ya hadhara na ndani; ruzuku ya serikali kwa vyama vya siasa; masuala ya uchaguzi; mfumo wa maridhiano ili kudumisha haki, amani na utulivu; ushiriki wa wanawake na makundi maalum katika siasa na demokrasia ya vyama vingi; elimu ya uraia, rushwa na maadili katika siasa; na uhusiano wa siasa na mawasiliano kwa umma.

Kuhusu mikutano ya kisiasa, alisema wanapendekeza kufutwa kwa kifungu cha 11(2) kinachotoa mamlaka ya matumizi ya vifungu vya 43 na 46 vya Sheria ya Jeshi la Polisi ya mwaka 1973 katika mchakato wa uitishwaji wa mikutano ya vyama vya siasa.

Kuhusu ruzuku kwa vyama vya siasa, alisema kuboreshwa kwa sheria kwa kuongezwa sharti la tengo la ruzuku kwa vyama vya siasa kuwa kati ya asilimia moja na mbili ya bajeti ya mwaka wa serikali.

"Asilimia 10 ya ruzuku igawanywe sawa kwa vyama vyote vya siasa vilivyokidhi masharti ya kifungu hicho, asilimia 40 igawanywe kwa vyama kwa uwiano wa viti vya wabunge wa kuchaguliwa, asilimia 25 igawanywe kwa vyama vya siasa kwa kuzingatia kura za wabunge na madiwani," aliwasilisha Semu.

# Mbunge alivyopiga sarakasi bungeni

**Augusta Njoji na Romana Mallya,**
DODOMA

MJADALA wa makadirio ya mapato na matumizi wa Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi kwa mwaka 2022/23 bungeni jana uliibua hisia kwa baadhi ya wabunge huku Mbunge wa Mbulu Vijijini (CCM), Flatei Massay, akiruka sarakasi ndani ya ukumbi wa Bunge na Mbunge wa Ukonga (CCM) Jerry Silaa, akimwaga machozi.

Katika sakata la kuruka sarakasi, Mbunge Massay akichangia mjadala huo alisema ameahidiwa mara nyingi kuhusu ujenzi wa barabara Mbulu hadi Hydom, lakini haijatekelezwa.

"Kamati ya Bunge ya Miundombinu imeonyesha fedha zilizotengwa mwaka jana kwa ajili ya ujenzi wa barabra hii katika kiwango cha lami zimepelekwa kulipa madeni, kama waliniahidi kuwa barabara itajengwa hili tangazo linachukua muda gani? Mimi hapa mheshimiwa Spika sio shilingi tu. Mimi wananchi wameniambia shilingi niichukue niende nayo Mbulu Vijijini maana hapa hamna namna tena," alisema.

"Mheshimiwa Spika wa Bunge (Dk. Tulia Ackson) kama hutanitoa nje ya ukumbi wa Bunge naomba kupiga sarakasi bungeni. Mimi naona wanataka kunitengenezea ajali kuliko kukitengenezea ajali chama changu si bora uruhusu tu niruke hapa ili washtuke sasa. Nitafanyaje sasa mheshimiwa Spika?" Alihoji.

Kutokana na baadhi ya wabunge kushabikia apige sarakasi, mbunge huyo alilazimika kupiga akitumia meza yake huku Dk.Tulia akimsihi kutofanya hivyo.

Akiendelea kuchangia, Massay alisema katika bajeti ya mwaka jana aliahidiwa kujengwa kwa barabara na ameuliza maswali saba mwaka jana na manne mwaka huu bila mafanikio.

Alisema yeye na wabunge wenzie saba walienda ofisini kwa Katibu Mkuu wa wizara hiyo kudai barabara.

"Wanafunzi wa jimboni kwangu hawajui barabara ya lami nililazimika kuwapeleka Babati kwa ajili ya kuona barabara ya lami, hata wananchi wangu wanaomba Mungu ukame wakati kunapokuwa na mvua labda ataelewa changamoto wanazopitia," alisema.

Naye Mbunge Silaa alisema Kampuni ya Syno Hydro, imepewa kazi ya ujenzi wa barabara ya mwendo kasi kutoka Gerezani hadi Mbagala, lakini iligundulika kuwa urefu wa kilometa 2.5 ulikuwa na ubovu.

"Pamoja na dosari hizi mkandarasi huyu amepewa zabuni ya kujenga barabara ya mwendo kasi kutoka Kariakoo hadi Gongo la Mboto yenye urefu wa Kilometa 23.6, kama viongozi wasingesimama na kusema hapa pabovu mkandarasi angeendelea huko, wakati mwingine serikali tuwe tunaangalia mkandarasi ana kazi zaidi ya moja na kwenye maeneo mengi wanavuruga,"

"Bunge lako hili linaenda kutekeleza kero hiyo hiyo ambayo iko Mbagala, iko Temeke litakuwa Bunge la namna gani? Mkuu wa Wilaya ya Temeke alikwenda kusimamia walipwe wafanyakazi, Tanroad (Wakala wa Barabara Nchini) wakamwandikia barua asiingilie mkataba huo."

"Mtu anaposema mapungufu haya huonekani kama ana jambo lake binafsi, sisi tunaenda kwenye uchaguzi," alisema huku akibubujika machozi na kukaa chini akiwa amefunika macho.

STEPMARK

**Makumbusho, PLOT No. 13 Block 45**
**P.O.Box 11767, Dar es salaam, Tanzania**
**Office : +255 715 300 312**
**E-mail: info@stepmark.co.tz**

## TANGAZO LA MINADA YA HADHARA!!

Step mark Limited kwa idhini tuliyopewa na **Benki ya CRDB Makao Makuu yaliopo Plot Namba. 25&26 Ally Hassan Mwinyi Road & Plot Namba.21.Barack Obama Road, S.L.P 268,11101 Dar es Salaam** tunatangaza minada ya hadhara wa kuuza mali mbali za wadaiwa wa **Benki ya CRDB** sehemu mbali mbali katika mikoa ya hapa Tanzania.

**Mali hizo zitauzwa kama zilivyo kwenye eneo kwa njia ya Minada ya hadhara..**

| S/No | JINA LA MDAIWA | AINA YA MALI | TAARIFA YA MALI INAYOUZWA | ENEO MALI ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Jotham Kifuja Mwasandube | GARI | Usajili namba. T140 DCU Chassis No: FK615E510094 Aina: FUSO Mchanganuo: Mitsubishi Aina ya Umbo: Dumper Usajili wa kadi: 6672879 | Tukuyu Almashauli ya willaya ya Rungwe | 09/06/ 2022 Saa Nne Asubui Miwsho Saa Kumi Jioni. |
| 2. | Joshia Daniel Magabe | NYUMBA | Eneo lisilopimwa | Mtaa: Mpomja Kata: Igawilo Jiji la Mbeya. | 10/06/2022 Saa Nne Asubui Miwsho Saa Kumi Jioni. |
| 3. | Gaston Asegelile Mwakasege | NYUMBA | Hati Namba 28315-MBYLR Ofisi ya Ardhi Namba 501743 | Plot Namba 106, Block"G"Igurusi Wilaya ya Mbalali | 12/06/2022 Saa Nne Asubui Miwsho Saa Kumi Jioni. |
| 4. | Paul Phares Mnyandwa | NYUMBA | Hati namba: 2124 Namba ya makazi: 1031860 | Ploti namba 413, Block V Unguu Road Gairo | 15/06/2022 Saa Nne Asubui Miwsho Saa Kumi Jioni |
| 5. | Said Salum Seif | NYUMBA | Hati Namba 23079-MBYLR Ofisi ya Ardhi Namba: 380953 | Plot Namba 98,Block "N"(HD) Bomani ,Manispaa ya Sumbawanga Mkoa wa Rukwa | 09/06/2022 Saa Nne Asubui Miwsho Saa Kumi Jioni. |
| 6. | Gasper Johnson Kiondo | NYUMBA | Hati Namba 89-RKLR Ofisi ya Ardhi Namba 791609 | Plot Namba 383,Block "T" Eneo la Kisiwani,Manispaa ya Sumbawanga Mkoa wa Rukwa | 11/06/2022 Saa Nne Asubui Miwsho Saa Kumi Jioni. |
| 7. | Ayubu Bononi Lwilla | NYUMBA | Hati namba: 208-RUKLR Namba ya Makazi 1149531 | Plot Namba 260 Blok AA (MD) Nkasisiwe, Manispaa ya Sumbawanga, Mkoa wa Rukwa | 13/06/2022 Saa Nne Asubui Miwsho Saa Kumi Jioni. |
| 8. | Apolinary Sipliano Selemani | NYUMBA | Eneo lisilopimwa | Kijiji cha Katani-Kata ya Nkandasi,Wilaya ya Nkasi Mkoa wa Rukwa | 15/06/2022 Saa Nne Asubui Miwsho Saa Kumi Jioni. |
| 9. | Apolinary Sipliano Selemani | NYUMBA | Eneo lisilopimwa | Kijiji cha Katani-Kata ya Nkandasi,Wilaya ya Nkasi Mkoa wa Rukwa | 15/06/2022 Saa Nne Asubui Miwsho Saa Kumi Jioni. |
| 10. | Apolinary Sipliano Selemani | NYUMBA | Eneo lisilopimwa | Kijiji cha Ninga,Wilaya ya Kalambo Mkoa wa Rukwa | 17/06/2022 Saa Nne Asubui Miwsho Saa Kumi Jioni. |
| 11. | Ivod G. Chalula | NYUMBA | Eneo lisilopimwa | Kalalasi,Wilaya ya Kalambo Sumbawanga Mkoa wa Rukwa | 18/06/2022 Saa Nne Asubui Miwsho Saa Kumi Jioni. |

**MASHARTI YA MNADA:**
1. Mnunuzi lazima afike eneo la mnada unapofanyika
2. Mnunuzi atalazimika kulipa asilimia ishirini na tano(25%) ya bei iliofikiwa papo hapo na asilimia sabini na tano (75%) atalazimika kulipa ndani ya siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe ya mnada na mteja akishindwa kulipa 75% ndani ya siku 14 atakua amepoteza haki ya ununuzi.

**KWA MAELEZO ZAIDI WASILIANA NASI KWA NAMBA +255 784068215 / 0719489940**

# Mbaroni kwa tuhuma za kuua akiamulia ugomvi

**Na Samson Chacha,** TARIME

MKAZI wa Kijiji cha Kewanja, Tarafa ya Ingwe wilayani Tarime, Samwel Samwel, anashikiliwa na polisi kwa tuhuma za mauaji ya watu wawili kwa kupiga risasi wakati akiamua ugomvi.

Waliofariki wametajwa kuwa ni Mwita Sibora na Chacha Bukima.

Kamanda wa Polisi Tarime Rorya, ACP William Mkonda, amethibitisha kutokea kwa tukio hilo na kueleza kuwa watu hao wote wakazi wa Nyamongo, wameuawa kwa kupigwa risasi na mtuhumiwa usiku wa kuamkia Jumapili wakati wakinywa pombe baa.

Alisema baada ya kutokea ugomvi kati ya Sibora na Bukima, Samwel aliyekuwa na silaha aina ya bastola alijaribu kuingilia ugomvi huo na kufyatua risasi moja hewani na zingine kuwapata watu hao na kusababisha vifo vyao papo hapo.

"Jeshi la Polisi tulifanikiwa kumkamata mtuhumiwa wa Samwel na tunamhoji zaidi kuhusiana na tukio hilo, baada ya uchunguzi tutamfikisha mahakamani kujibu mashtaka yanayomkabili," alisema kamanda.

Alitoa wito kwa wamiliki wa baa kuwakagua wateja wao kama wana silaha na kuisalimisha hadi wanapotaka kuondoka wakabidhiwe, kutokana na kujitokeza kwa matukio mengi ya watu wenye silaha za moto sehemu za vilevi na kusababisha madhara.

Alisema miili ya marehemu hao imepelekwa kufanyiwa uchunguzi na imehifadhiwa chumba cha maiti Kituo cha Afya Sirari kabla ya kukabidhiwa kwa ndugu zao.



Ofisa Uhusiano wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Avitus Rushaka (kulia), akimsikiliza na kuchukua taarifa za mfanyabiashara wa duka la reja reja wilayani Kilosa jana, katika kampeni ya elimu kwa mlipakodi mlango kwa mlango iliyoanza jana mkoani Morogoro. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Ndumbaro aahidi kasi utoaji haki mahakamani

**Na Grace Gurisha**

WAZIRI wa Katiba na Sheria, Dk. Damas Ndumbaro, amesema kasi ya maboresho ya Mahakama itakwenda sambamba na utoaji haki kwa haraka kwa kuwa hivi sasa kesi zinasikilizwa na kutolewa uamuzi kwa haraka baada ya maboresho yaliyofanyika.

Dk. Ndumbaro alisema hayo jana, jijini Dar es Salaam alipotembelea Mahakama ya Tanzania na kufanya mazungumzo na Jaji Mkuu wa Tanzania, Profesa Ibrahim Juma, ikiwa ni moja ya ziara yake ya kikazi tangu alipoteuliwa kuwa waziri.

Alisema katika mazungumzo yao, Profesa Juma amemhakikishia kwamba kasi ya maboresho inaendelea kwa kasi kubwa kwa lengo la kuhakikisha haki inatendeka na ionekane inatendeka.

Pia alisema Profesa Juma amemhakikishia ushirikiano, kama inavyofahamika Mahakama ni muhimili ambao uko huru kwa mujibu wa Katiba hauingiliwi na mingine.

Alisema muhimili wa Mahakama utaendelea kutoa ushirikiano katika mambo ya kisera katika wizara hiyo.

"Nimepata fursa ya kutembelea Mahakama ya Tanzania nikiwa Waziri wa Katiba na Sheria, ambapo Profesa Juma ameniahidi ushirikiano na amenieleza kwa jinsi gani mahakama imefanya maboresho katika utoaji haki kuwafikia wananchi."

"Naifahamu mahakama, ulikuwa ukitembea mahakamani hata kupata faili ilikuwa ngumu sana, mafaili yamerundikana tu na majengo hayajaboreshwa, lakini leo ukitembelea mahakama yoyote unaona mfumo wao wa mafaili ni mzuri sana wameingiza kwenye huduma za kidigitali kupitia Mahakama," alisema Dk. Ndumbaro.

Akizungumzia suala la uchache majaji, alisema katika uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan ndani ya mwaka mmoja amefanya uteuzi wa majaji wengi hasa wanawake na kuahidi watakuwa wengi zaidi.

# PSC yapewa agizo kushughulikia rufani haraka

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

NAIBU Waziri, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, Deogratius Ndejembi, ameagiza Tume ya Utumishi wa Umma (PSC) kushughulikia haraka rufani na malalamiko ya watumishi ambao hawajaridhishwa na uamuzi wa mamlaka zao za nidhamu.

Ndejembi alitoa kauli hiyo jana jijini hapo alipokuwa akizindua Tume hiyo pamoja na mafunzo ya siku tatu ya wajumbe wapya wa tume hiyo.

Alisema hatua hiyo itaondoa tatizo la rufani hizo kucheleweshwa na kukaa muda mrefu.

"Wajumbe wa Tume hii mnatakiwa mara moja kuanza kushughulikia rufani na malalamiko ya watumishi na kutolea uamuzi mapema," alisema.

Ndejembi aliwaasa kutenda haki kwa watumishi ambao wanakuwa wamekata rufani kutokana na kutoridhishwa na uamuzi uliotolewa na mamlaka za ajira na nidhamu.

Hata hivyo, alisema kanuni za Tume hiyo zilizotungwa mwaka 2003 zinafanyiwa marekebisho ili kuiruhusu kutoa uamuzi kwenye rufani hata bila kupata vielelezo vya upande wa pili.

"Niagize waajiri, mamlaka za ajira na taasisi nyingine zinazohusika na watumishi, kuhakikisha zinawasilisha vielelezo vya walalamikaji kwa tume ili ishughulikie haraka rufani na malalamiko ya watumishi hao kwa wakati," alisema.

Kwa upande wake, Mwenyekiti Tume hiyo, Hamisi Kalombola, alisema, aliahidi yeye na makamishna watatimiza wajibu wao kwa kufuata sera, sheria, taratibu, kanuni na miongozo na maelekezo ili kutoa huduma bora kwa watumishi.

Katibu Mkuu wa Tume hiyo, Mathew Kirama, alisema uteuzi wa makamishna wa tume hiyo umezingatia uwezo, uadilifu na uzalendo wao kwa taifa.

# Kituo watoto wenye usonji chakabidhiwa milioni 4.1/-

**Na Mary Geofrey**

TAASISI ya Lukiza Autism, imekabidhi hundi ya Sh. milioni 4.1 kwa Kituo cha Ufundi cha Watoto wenye changamoto za ufahamu cha Salt, kilichoko Mbezi Makabe, mkoani Dar es Salaam.

Msaada huo ni miongoni mwa madhumuni ya mbio za hisani (Run 4 Autism inclusive Marathon 2022) zilizofanyika Aprili 10, mwaka huu.

Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Lukiza Autism, Hilda Nkabe, alikabidhi msaada huo jana pamoja na medali kwa waandishi wa habari ikiwa ni kutambua mchango wao katika kuandika habari za watu wenye ulemavu.

Alisema msaada waliotoa ni moja ya utekelezaji wa malengo ya taasisi yake ya kuwasaidia vijana wenye usonji na ulemavu mwingine kupata ujuzi wa kilimo mahiri ili kujipatia chakula na kujihusisha kwenye shughuli za kiuchumi.

"Fedha hizi tulizipata katika mbio tulizozifanya za kuelimisha jamii kuhusu usonji ilikuwa ni uadhimishaji wa mwezi wa kuelimisha jamii kuhusu usonji duniani, kuelimisha jamii juu ya ujumuishwaji wa watu wenye changamoto ya ugonjwa huu katika shughuli zote za afya, elimu, kiuchumi na kijamii.

"Kuhamasisha familia zenye watoto wenye usonji na ulemavu mwingine, kutowaficha na kuchangisha fedha za kusaidia kituo hiki, nalo tumefanikiwa leo," alisema.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Kituo cha Salt, Rebecca Lebi, alisema fedha hizo zitatumika kuendeleza mradi wa kilimo mahiri cha mjini (intensive urban farming) na utajumuisha ufugaji wa samaki kwa njia ya matangi, kilimo cha mboga kwa matone na ufugaji wa kuku wa kienyeji.

Alisema zitasaidia mradi huo kuanza mara moja kwa kununulia vifaa na pembejeo, kupata mboga, kuku na samaki salama kwa ajili ya matumizi ya kituo na kuuza ili kujipatia fedha za kulipia bili za maji na umeme.

**"Kuhamasisha familia zenye watoto wenye usonji na ulemavu mwingine, kutowaficha na kuchangisha fedha za kusaidia kituo hiki, nalo tumefanikiwa leo," alisema.**

# Bashungwa aonya vikundi hewa kupewa mikopo ya h'shauri 10%

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Innocent Bashungwa, ameonya vikundi hewa na watu wasio walengwa kwenye mikopo ya asilimia 10 ya mapato ya ndani ya halmashauri inayotolewa kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

Akifungua mafunzo ya mfumo wa usimamizi wa mikopo hiyo jana jijini hapo, Waziri Bashungwa alisema uwapo wa mfumo huo ni njia sahihi ya kutekeleza maelekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali (CAG), kuhusu fedha hizo kutokana na hoja hiyo kuwa ikijirudia huku kamati za Bunge zikitoa mapendekezo kuhusu usimamizi kila mwaka.

Alisema baada ya mafunzo hayo hataki kusikia fedha hizo zinakwenda kwa vikundi hewa au kwa watu wasio walengwa.

"Mheshimiwa Katibu Mkuu (Prof. Riziki Shemdoe) kwenye mafunzo haya masuala ya vikundi hewa lazima yajadiliwe na tutoke na mkakati wa kuyadhibiti yaani iwe historia tusisikie mambo ya vikundi hewa, watu wasiolengwa kupata mikopo hii lazima mfumo huu na kikao kazi hichi kiangalie."

"Baada ya mafunzo haya hatutaki kusikia watu wasiolengwa wanapata mikopo, baada ya mafunzo haya lazima watoke na mbinu za maarifa yalioyopatikana kwenye mafunzo tuone wanavyokwenda kufuatilia vikundi ambavyo vimepata mikopo na kuhakikisha mikopo waliyopata inakwenda kuwasaidia kubadilisha maisha yao, na sio kuwapa mikopo ilimradi tu," alisema.

Alisema fedha zinazokwenda kwenye vikundi ziwe na tija kwa kubadili maisha yao.

"Pia, mkaangalie urejeshaji ili vikundi vingine viweze kupata, lazima kikao kikazi hiki na majibu yapatikane," alisema. Bashungwa alitaka wataalamu hao kupitia sheria na kanuni za utoaji mikopo hiyo ili kuenda sambamba na mfumo huo na endapo kuna upungufu wizara yake itafanya marekebisho ya sheria.

Kadhalika, alimwagiza Katibu Mkuu TAMISEMI, kuimarisha Sekretarieti za Mikoa na Wilaya ili kusimamia kwa karibu wa miradi ya maendeleo kwenye maeneo yao.

"Katibu Mkuu pia hakikisha unaimarisha mifumo iliyopo ili kuongeza ufanisi wa utendaji kazi ikiwamo mfumo wa TAUS," alisema.

Akizungumzia barabara za mitaani, Bashungwa alimwagiza Katibu Mkuu huyo kusimamia mwongozo unaotaka halmashauri zinazokusanya zaidi ya Shilingi bilioni tano zinatenga asilimia 10 kwa ajili ya kutengeneza barabara za mitaa.

Awali, Katibu Mkuu, Profesa Shemdoe alisema Ofisi ya Rais-TAMISEMI imekuja na mfumo huo wa kielektroniki kutafuta njia bora ya kuhakikisha fedha za asilimia 10 kwa vikundi zinakusanywa, zinatumika na zinarejeshwa.

Kwa upande wake, Mkuu wa Idara ya Mahusiano, Ofisi ndogo ya Dodoma wa Benki ya NMB, Vicky Bushumbo, alisema benki yake imeamua kushiriki kuandaa mfumo huo baada kubainika kuna tatizo la udhibiti utoaji na urejeshaji wa mikopo hiyo.

"Benki imetoa takribani Sh. milioni 130 katika kuhakikisha tunasaidia uboreshaji wa mfumo huu na Sh. milioni 10 kwa ajili ya mafunzo ya mfumo huu ili kusaidia watendaji kupata urahisi wakati wa utoaji na urejeshaji mikopo," alisema.




Mkuu wa Mauzo Vodacom Tanzania PLC Kanda ya Ziwa, Ayubu Kalufya (kushoto), akisalimiana na Mkurugenzi Msaidizi wa Tiba Asili na Tiba Mbadala wa Wizara ya Afya, Dk. Paulo Mhame, katika maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Kutokomeza Ugonjwa wa Fistula, sambamba na kuzinduliwa mwongozo wa kitaifa kuhusu fistula, jijini Mwanza jana. Kulia ni Mkurugenzi wa Hospitali ya Bugando, Fabian Masaga. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Rais Samia kupokea tuzo Ghana

**Na Maulid Mmbaga**

RAIS Samia Suluhu Hassan, anatarajia kupokea tuzo ya mwaka ya Babacar Ndiaye, kutokana na mafanikio ambayo serikali yake imeyapata katika ujenzi wa miundombinu ya usafirishaji.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Kaimu Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais Ikulu, Jaffar Haniu, Rais aliondoka nchini jana na kuelekea Accra, Ghana kwa ziara ya kikazi ya siku tatu.

"Rais anatarajia kupokea tuzo hiyo ambayo hutolewa kwa mkuu wa nchi iliyofanya vizuri na hutolewa kila mwaka katika mkutano wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AFDB) ambao kwa mwaka huu unafanyia Accra, Ghana," alisema Haniu. Aliongeza kuwa katika mkutano huo Rais pia anatarajia kushiriki mdahalo wa wakuu wa nchi utakaojadili fursa mbalimbali zilizomo na changamoto zinazokabili nchi za Afrika.

Aidha, alibainisha changamoto hizo zitakazojadiliwa ikiwamo mabadiliko ya tabianchi, kupanda kwa bei ya vyakula na matumizi ya nishati endelevu.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Mabadiliko kwenye sheria yalete manufaa

**SERIKALI** imesema inatarajia kutengeneza ajira mpya milioni nane hadi mwaka 2025 kwa kufanya mabadiliko ya sheria, sera na kanuni za uwekezaji ambazo kwa kiasi kikubwa zimeonekana kukwaza ustawi wa sekta hiyo.

Pia imeahidi kufanyia kazi mapitio ya sheria, sera na kanuni za biashara nchini, lengo likiwa ni kutengeneza sekta binafsi imara yenye kuchangia uchumi wa mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla.

Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, Dk. Ashatu Kijaju, alisema lengo la serikali ni kujenga mazingira wezeshi kwa kuondoa vikwazo vyote, ikiwamo kodi korofi ambazo zimedhoofisha uwekezaji na kusababisha sekta hiyo kushindwa kufikia malengo tarajiwa.

Kauli ya waziri inakuja wiki chache baada ya Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Profesa Godius Kahyarara, wakati wa uzinduzi wa filamu ya Royal Tour, kuwa alieleza katika majadiliano na wawekezaji mbalimbali walibaini sheria, sera na kanuni nyingi zimepitwa na wakati zinahitaji kubadilishwa.

Alisema nyingi ni za miaka ya 90 ambayo sio mbali na 60 na sasa tupo miaka ya 2022, jambo linaloonyesha kuna mambo hayakuwa yamejumuishwa kwa ajili ya kuwezesha wawekezaji kufanyabiashara nchini kwa kutoa ajira, kuchangia uchumi wa nchi na mtu binafsi. Hii ni habari njema hasa kwa wakati huu ambao Tanzania inajijenga upya baada ya kupitia kipindi ambacho hakikuwa rafiki kikodi na kisiasa, hali iliyosababisha wengi kufunga biashara au kufungasha virago.

Baada ya kuingia madarakani Rais Samia Suluhu Hassan, aliwataka Uwekezaji na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), kufanyakazi ya ziada kuondoa vikwazo vyote, kuacha kuchukua fedha kwenye akaunti za watu, kukamata wafanyabiashara na kufunga biashara.

Hatua zinazochukuliwa sasa ni za kupongezwa kwa kuwa zinakwenda kuistawisha sekta binafsi ambayo duniani kote imekuwa ni kiini cha uchumi kwa kuwa ndiyo walipa kodi wakubwa na walioajiri wengi.

Duniani kote ajira nyingi zipo sekta binafsi, serikali hazifanyi biashara (kutegemea na sheria za nchi husika), inabaki kuwa mwezeshaji kwa kuhakikisha sera, sheria na kanuni ni zenye kukuza uchumi, ndicho kilichoonekana kwa sasa kwamba serikali imeliona tatizo kwa upande wao wanalirekebisha.

Kwa mujibu wa sheria zetu Rais ndiye Mwenyekiti wa Baraza la Biashara Tanzania, ambalo hukutana kila mwaka kujadili mambo mbalimbali ya kukuza biashara na uchumi wa nchi.

Wakati wa utawala wa Rais Jakaya Kikwete, alitumia muda mwingi kujenga sekta binafsi imara na mara zote alisisitiza kuwa ndiyo injini ya uchumi wa nchi, alihakikisha inakuwa na Watanzania wengi walio ajiriwa.

Tunaipongeza Serikali ya Rais Samia kwa kuona hili na sasa inainyanyua sekta hii ili kufikia lengo la ajira milioni nane miaka mitatu ijayo, maana yake nchi inakwenda kupata kodi za biashara, kampuni, taasisi na watu binafsi.


Lazima serikali itimize wajibu wake wa kujenga mazingira wezeshi sekta binafsi ikifanikiwa katika hilo itaongeza makusanyo ya kodi, ajira na kustawi kwa uchumi.

Pamoja na yote mazuri tunakumbusha serikali kuweka jicho lake wazi kila sekunde kuhakikisha uwekezaji unaofanyika nchini unanufaisha Watanzania.

Mathalani, uwekezaji kwenye maliasili muhimu kwa nchi yetu, kuzijua siasa za dunia (Geo Politics), ambazo wakati mwingine huziumiza nchi maskini, lazima watendaji serikalini wawe mbele ya wawekezaji wowote kwa maslahi mapama ya nchi.

Lazima tuwe na uwekezaji wenye uwajibikaji, tuone vyombo vya wafanyabiashara kama Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF), vinasimama imara kutetea maslahi ya nchi pasipo kutanguliza maslahi binafsi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Uwekezaji utafiti utatatua matatizo mashambani

Na Mwandishi Wetu

**SERIKALI** ya awamu ya tano na sasa ya sita imejikita katika kampeni ya kuwa na Tanzania ya viwanda, lakini kufundisha na kuandaa wasomi wa sayansi ili kupeleka maendeleo ya sayansi na teknolojia kwa Watanzania.

Sambamba na kuimarisha viwanda serikali, inakusudia kufikisha nchi kwenye uchumi wa kati kwa kuwa na viwanda vipya vya kisasa zaidi, kufufua vilivyokwama ili kufanya kazi tena na kuhamasisha wawekezaji kuja nchi kufungua miradi ya kiuchumi.

Kuwekeza kwenye viwanda kunategemea wasomi na watafiti na hilo halikuachwa nyuma, serikali inajenga shule za sayansi kwa kila mkoa kwa ajili ya kufundisha wasichana ili taifa liwe na wasomi wanasayansi kinamama.

Ni jambo jema na la muhimu kuwekeza na kuwa na taasisi imara za kitafiti zinazoweza kuuhamisha utafiti kutoka maabara na kuufikisha kwa wananchi vijijini ili kitendawili cha kuwa na uchumi wa viwanda kuteguliwa.

Hivyo, kuwekeza katika teknolojia ni muhimu na kuanzisha uwekezaji mkubwa wa kiutafiti hasa kwenye kuboresha kilimo ambacho ndicho mzalishaji mkubwa wa malighafi za viwanda hivyo.

Tanzania inahitaji kukabiliana na changamoto za uzalishaji mashambani ili kuiwezesha nchi kuwa na malighafi za kutosha viwandani, utoshelevu wa chakula na kutibu hali ya mazingira inayoharibiwa na kilimo kisichojali mazingira.

Utafiti ni vyema uanze kuelekezwa kwenye kilimo ambacho sasa kipo taabani kutokana na ukame, wadudu waharibifu na matumizi makubwa ya viuatilifu ambavyo vinatishia afya za walaji na mazingira.

Baadhi ya mikoa wakulima wakubwa wa mahindi, mboga na matunda wanalizwa na wadudu waharibifu wa mazao.

Mathalani, wadudu wanashambulia mboga na kuwalazimisha wakulima kutumia viuatilifu vingi kupindukia bila mafanikio.

Mahindi yanashambuliwa na kusababisha hasara ya mabilioni ya pesa kila mwaka na kinachohitajika ni uwekezaji kwenye utafiti na kutambua aina za wadudu ili kuwadhibiti.

Utafiti huo ni vyema uanze kutengeneza dawa za asili ili kupunguza matumizi ya kemikali za viwandani.

Ikumbukwe viuatilifu vya viwandani ni sumu inayoathiri kila mmoja ambaye anaweza kukutana nayo katika vyakula, hewa anayovuta na maji anayotumia.

Hivyo basi, kuna kila sababu ya kuunga mkono jitihada za serikali katika suala la kuwekeza kwenye utafiti na kusomesha wataalamu wenye uwezo wa kusimamia viwanda na kazi za kutafiti.

Kuwapo na wataalamu kunamaanisha kuajiriwa Watanzania walio na sifa za kusimamia viwanda hivyo na kufanya utafiti huku wakisimamia viwanda.

Wataalamu watafanya utafiti kwa kupima virusi, vimelea na wadudu mbalimbali wanaoshambulia mazao.

Lakini pia, kupitia utafiti watatengeneza mbegu zenye ukinzani na virusi, wadudu na viwavi baada ya kutambua aina ya virusi na mahali vinapopatikana

Watafiti hao na watalaamu watasaidia kufunza wakulima mbinu za kutumia kanuni za kilimo bora na kustawisha mazao ili kupata tani nyingi za mazao hayo ikiwa ni kuzalisha malighafi za kutosha viwandani.

Ni wataalamu na watafiti watakaofanikisha kusambaza mbegu kimkakati ili kudhibiti magonjwa badala ya kutibu mazao yakiwa yameathirika.

Utafiti utawezesha wakulima kumiliki viwanda vyao, kuwa na soko la mazao yao na kupunguza umaskini hivyo Watanzania kunufaika na kilimo chao mashambani.

Changamoto za kukosekana wataalamu zitamalizika kwa kuwekeza kwenye masomo ya sayansi, kuandaa walimu, maabara na vifaa vya kutosha vya maabara katika shule hizo maalumu.

Wimbo wa Tanzania ya viwanda inawezekana utakuwa na uhalisia kama taifa litawekeza na kuimarisha utafiti unaotatua matatizo hasa kwenye kilimo ambacho ni uti wa mgongo wa uchumi wa taifa.

## Wiki ya Maziwa kuangalia makundi maalum

**Na Neema Hussein,** KATAVI

KUELEKEA maadhimisho ya 25 ya Wiki ya Maziwa ambayo mwaka huu kitaifa yanafanyika mkoani Katavi, jamii imetakiwa kuitumia fursa hiyo kujifunza namna ya ufugaji bora wa ng'ombe kwa lengo la kuongeza uzalishaji nchini.

Wito huo ulitolewa na Mkuu wa Mkoa wa Katavi, Mwanamvua Mrindoko, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuelekea maadhimisho hayo yanayotarajiwa kuanza Mei 27, 2022 hadi Juni Mosi, 2022.

Aidha, Mrindoko alisema, lengo la maadhimisho hayo ni kuboresha unywaji wa maziwa kwa ugawaji kwenye makundi maalumu vikiwamo vituo vya kulelea watoto yatima, wazee na magereza.

"Lengo ni kuboresha unywaji wa maziwa na bidhaa zake na soko lake," alisema Mrindoko.

Alisema maadhimisho hayo yamekuwa yakilenga kutoa elimu kwa umma ya matumizi ya maziwa na faida zake, kuwaelimisha wadau kuongeza ubora wa bidhaa hiyo inayotengenezwa nchini, kuwashawishi watunga sera umuhimu wa tasnia ya maziwa katika kukuza uchumi wa nchi na kuondoa umaskini.

Mrindoko alisema sababu ya maadhimisho hayo kufanyika kitaifa mkoani Katavi inatokana na mapendekezo ya wadau wa tasnia ya maziwa nchini kwa kuzingatia uwekezaji mkubwa katika sekta hiyo unaohitajika katika Mkoa wa Katavi.

Kihistoria Wiki ya Maziwa ilianzishwa na Shirika la Chakula Duniani (FAO), ambao walichagua wiki hiyo kuwa ya uhamasishaji wa unywaji maziwa duniani kwa kuzingatia kuwa ni chakula bora kwa watu wa rika zote na ni mlo ulio kamili.

Tanzania utaratibu wa kuadhimisha wiki ya unywaji wa maziwa ulinzishwa na Chama cha Wafugaji wa Ng'ombe wa Maziwa Pwani na Dar es Salaam (CODAFA) Juni 1997 baada ya mkutano wa Kanda ya Afrika Mashariki na Kati kwa ufadhili wa Shirika la Land O' Lakes baada ya wazalishaji na wasindikaji kukosa mahali pa kuuzia.

# Mwingine auawa kwa risasi mgodi wa almasi

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

HAMIS Mayunga (27), mkazi wa Kijiji cha Dulisi wilayani Kishapu mkoani Shinyanga, amedaiwa kuuawa kwa kupigwa risasi na mlinzi wa kampuni ya Sam Security, Chacha Emmanuel wa mgodi wa almasi wa El-Hilali.

Kamanda wa Polisi mkoani Shinyanga, George Kyando, akitoa taarifa kwa vyombo vya habari jana, alisema tukio hilo lilitokea Mei 20, mwaka huu majira ya saa 4 usiku.

Alidai kuwa Hamis alikuwa na wenzake zaidi ya 10 wakivua samaki katika bwawa lililoko ndani ya mgodi huo wa El-Hilali na walinzi hao walipofika na kuwazuia kuvua, waligoma na hivyo kukatokea kutoelewana na kusababisha mauaji hayo.

"Wakati mzozo ukiendelea kwenye bwawa hilo ndipo mlinzi mmoja, Emmanuel Chacha akiwa na wenzake wanne, akampiga risasi upande wa kushoto kwenye moyo na kufariki dunia papo hapo," alisema Kyando.

Alisema baada ya tukio hilo, mlinzi huyo alikimbia kusikojulikana na kuitelekeza bunduki aliyokuwa nayo aina ya shortgun na jeshi hilo linamtafuta ili afikishwe mahakamani kwa hatua zaidi za kisheria.

Alisema jeshi hilo pia linawashikilia walinzi wenzake wanne kwa ajili ya upelelezi juu ya tukio hilo na kutoa wito kwa kampuni za ulinzi kuacha matumizi holela ya silaha.

Alisema hilo ni tukio la pili kutokea mkoani Shinyanga ndani ya mwezi mmoja walinzi wa migodi kusababisha mauaji. Tukio lingine lilitokea kwenye mgodi wa Mwakitolyo wilayani Shinyanga, Jackson Joseph (35) aliuawa na mlinzi wa kampuni binafsi Mei 17, mwaka huu.

Kamanda huyo alitoa wito kwa wananchi ambao wanazunguka migodi ya madini kutii sheria na kuacha kuingia kwenye maeneo ambayo yanalindwa.




Ofisa Mkuu wa Wateja Binafsi na Biashara wa Benki ya NMB, Filbert Mponzi (watatu kushoto), akizungumza na mfanyabiashara wa mboga katika soko la Kilombero jijini Arusha, Ally Shabani (wapili kulia), baada ya kuzindua kampeni ya Teleza Kidigitali kwa Kanda ya Kaskazini. Kulia ni Meneja wa NMB Kanda ya Kaskazini, Dismas Prosper na Ofisa Mauzo NMB, Grace Fungo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Afariki dunia kwa kugonga kiberenge Morogoro

**Na Idda Mushi,** MOROGORO

MWENDESHA baiskeli maarufu mjini Morogoro, Michael Mgombera, pia anajulikana kama Mwarabu Fighter, amefariki dunia na mwingine kujeruhiwa baada ya gari waliyokuwa wakisafiria aina ya Toyota Hilux Pick Up kugonga kiberenge katika eneo la makutano ya reli Kilimahewa, mjini hapa usiku.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, SACP Fortunatus Musilim, amekiri kutokea ajali hiyo ambayo imehusisha gari ndogo yenye namba ya usajili T 840 DQF aina ya Toyota Hilux iliyogonga kiberenge kinachomilikiwa na Shirika la Reli Tanzania (TRC). Musilim alisema ajali hiyo ilitokea saa sita usiku na kusababisha kifo cha dereva wa gari ndogo ambaye ndiye mmiliki wa gari hiyo na kwamba kiberenge kilikuwa kikitokea Kilosa kuelekea stesheni ya Morogoro.

"Katika gari hiyo kulikuwa na watu wawili na majeruhi mmoja, Razia Kassim, ambaye emepelekwa Hospitali ya Mkoa wa Morogoro kwa matibabu na dereva ambaye alipoteza maisha papo hapo eneo la tukio," alisema Musilim.

Alitaja chanzo cha ajali hiyo kuwa ni uzembe wa dereva wa gari dogo kutaka kupita bila tahadhari maeneo ya makutano ya reli licha ya dereva wa kiberenge cha treni kupiga king'ora kama tahadhari ya ki usalama kwa wapita njia wengine.

"Dereva wa gari alikuwa hayupo makini ni kwamba hakuchukua hatua yoyote wakati alipofika katika eneo la makutano ya reli," alisema Kamanda.

Kwa mujibu wa mashuhuda wa ajali hiyo, saa sita usiku wakati wakiwa kwenye harakati za kutafuta maisha, walikuta gari imebamizwa na kiberenge cha treni na kusikia sauti ya mwanamke akilia kuomba msaada.

"Wakati natoka Msamvu kwenda maeneo ya Tumbaku nilisikia sauti ya mwanamke analia kutaka msaada ndipo watu tunasogea kuanza kumsaidia kwa kushirikiana na polisi na askari wa Zimamoto," alisema mmoja wa mashuhuda, Hassan Hassan.

Shuhuda mwingine alisema mwanamke aliyekuwa na marehemu, aliokolewa majira ya saa 11 alfajiri tangu ajali kutokea, alibanwa na chuma za gari na kushindwa kumtoa marehemu Mgombera hadi gari iliponyanyuliwa.

"Huyu dada alilia sana hadi kupoteza fahamu, toka saa 6.30 usiku, saa 11 ndiyo tukamuokoa, aliishiwa nguvu kabisa, ni mkazi wa Mafiga, mkono mmoja uliingia kwenye siti, kijana mmoja fundi alikuja akajiminya akaingia kukata siti kwa tabu kubwa, mwanzo tuliwaza tumkate mkono kumuokoa, awali alikuwa amebanwa na vyuma, anaita niokoeni...niokoeni, Fire (Zimamoto) waliogopa kutumia hata greda, maana yake unatumia petroli, ingeweza kuleta shida zingine," alisema mmoja wa mashuhuda ambaye hakutaka kutajwa jina lake.

# Mahakama ya Rufani yatupa maombi ya mfanyabiashara

**Na Grace Gurisha**

MAHAKAMA ya Rufani imetupilia mbali maombi ya marejeo ya mfanyabiashara Jitesh Ladwa, aliyekuwa akipinga uamuzi wa Mahakama Kuu kwamba ilikosea kutoa uamuzi wa kukubali maombi ya wanafamilia wenzake kwamba hana uhalali wa kusimamia uendeshaji wa Kampuni ya Indian Ocean Hotels Limited inayomiliki hoteli maarufu ya Golden Tulip.

Uamuzi uliotolewa na jopo la majaji, Dk. Gerald Ndika, Penterine Kente na Othman Makungu, ulieleza kuwa sheria inayoipa mamlaka ya kusikiliza rufani, inazuia rufani au maombi ya marejeo dhidi ya uamuzi au amri ndogo za mahakama ambazo hazina matokeo ya kumaliza shauri.

Mahakama ilisema sababu zilizotolewa na mrufani hazikidhi sifa za msingi za kuomba maombi ya marejeo.

Mahakama hiyo ilisema hakuna rufani au maombi ya mapitio ambayo yatakubaliwa dhidi ya uamuzi wa Mahakama Kuu, uamuzi wa awali au uamuzi mdogo au amri, isipokuwa tu kama uamuzi au amri hizo matokeo yake huhitimisha shauri.

"Hatuwezi kuona sababu ya msingi kwa nini leo tugeuke na kutoa tamko la kimahakama kinyume cha msimamo sahihi wa sheria ulioelezwa hapo juu, ambao tayari tumeshautamka sisi wenyewe.

"Lakini sababu zilizotolewa na waombaji hazikidhi matakwa ya chini ambayo yangeifanya mahakama kurejea uamuzi wake wa awali. Hatima yake tunayafutilia mbali maombi haya kwa gharama," lilisema jopo hilo.

Katika uamuzi wa Mahakama Kuu Divisheni ya Biashara, uliotolewa na Jaji Deo Nangela, alikubaliana na hoja za wadai huku Jitesh hakukubaliana na uamuzi huo na kufungua maombi ya mapitio Mahakama ya Rufani akiomba ipitie uamuzi huo wa Mahakama Kuu kwa madai kuwa mahakama hiyo ilikosea katika uamuzi wake. Wanafamilia hao walifungua kesi ya kibiashara Mahakama Kuu Divisheni ya Biashara dhidi ya Jitesh na kampuni hiyo ya Indian Ocean Hotels Limited, wakiomba amri sita ikiwamo mahakama hiyo itamke kuwa mwenendo na uendeshaji au utendaji wa Jitesh kwa kampuni hiyo haukuwa halali na aliathiri maslahi ya kampuni na wadai kama wanahisa, wakurugenzi na wajumbe wa kampuni.

Waliomba imzuie Jitesh kutokushiriki katika menejimenti ya masuala ya kampuni na amri ya kuielekeza menejimenti ya kampuni kukabidhiwa kwa waombaji.

Pia imlazimishe Jitesh kuachia ofisi na eneo la biashara ili itumiwe na kampuni tu na hasara ya jumla kwa waombaji kwa kadri ya tathmini ya mahakama.

Pia kumlazimisha Jitesh kuhusika kwa hasara zote na zilizopatikana kama matokeo ya matumizi mabaya ya fedha na usimamizi mbaya wa kampuni uliofanywa na mjibu maombi wa kwanza.




Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe (kulia), akikabidhiwa zawadi na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB), Frank Nyabundege, alipotembelea banda la maonyesho la TADB bungeni jijini Dodoma, wakati wa hotuba ya bajeti ya Wizara ya Kilimo iliyopitishwa mapema wiki hii. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Uelewa mdogo sheria kikwazo ukusanyaji wa mapato Pwani

**Na Julieth Mkreri,** KIBAHA

HALMASHAURI ya Mji wa Kibaha inakabiliana na kikwazo cha uelewa mdogo katika ukusanyaji wa mapato kutokana na uelewa mdogo wa sheria na taratibu za uendeshaji biashara mbalimbali.

Kwa mujibu wa Kaimu Mkurugenzi wa halmashauri hiyo, Optuna Kasanda, baadhi ya wafanyabiashara huona kama wanaonewa wanapotakiwa kufuata sheria.

Kasanda aliyabainisha hayo juzi wakati wa kikao cha Baraza la Madiwani alipokuwa akitoa taarifa ya utekelezaji wa kazi za idara ya fedha na biashara kwa kipindi cha mwezi Julai hadi Machi 2022.

Alisema kikwazo kingine ni pamoja na baadhi ya wafanyabiashara wa soko la Mnarani kuendelea kufanya biashara katika eneo la Mailimoja Stendi, lakini mfumo mpya wa ulipaji serikalini (MUSE) kuwa kikwazo kutokana na upya wake.

Kasanda alisema mikakati ya halmashauri hiyo ni kuendelea kuwajengea uwezo wafanyabiashara na wajasiriamali ili kutekeleza sera za kisekta kufikia dira ya maendeleo ya mwaka 2025.

Alibainisha kuwa kwa kipindi cha robo tatu, halmashauri hiyo kwa kushirikiana na wadau wamekusanya mapato ya ndani Sh. 1,030,880,849 na kufanya mapato ya kuanzia Julai 2021 hadi Machi 2022 kufikia Sh.3,999,623,748.92 sawa na asilimia 97 ya makisio ya mwaka 2021/2022 ambayo ni Sh. bilioni 4.1.

Kaimu Mkurugenzi huyo pia alisema kuwa kwa robo zote tatu kuanzia Julai hadi Machi 2022, halmashauri hiyo imekusanya mapato toka kwenye vyanzo fungwa Sh. 257,374,923.09 na kufanya jumla ya mapato yote ya ndani na vyanzo fungwa kuwa Sh. 4,256,998,672.01 sawa na asilimia 93 ya makisio ya mwaka 2021 ambayo ni Sh. 4,561,367.650.

Kasanda alisema halmashauri hiyo kwa kushirikiana na wakuu wa idara na vitengo pamoja na timu za ufuatiliaji wa mapato wanafanya zoezi la ufuatiliaji, ukaguzi na usimamizi kwa walipakodi na ushuru.

## Waanzisha kampeni kuepuka maambukizi UVIKO

**Na Sabato Kasika**

KITUO cha Sauti ya Jamii Kipunguni, jijini Dar es Salaam kwa kushirikiana na wadau wa afya wa Kata ya Kipunguni, kimeanzisha kampeni iitwayo 'Jihadhari na kamba ya kisima' inayolenga kuepusha watu na ugonjwa wa UVIKO-19.

Hayo yalisemwa na Mkurugenzi wa kituo hicho Seleman Bishagazi, alipokuwa akizungumza na gazeti hili jana na kufafanua kuwa kampeni hiyo pia inagusa kuepusha watu na magonjwa mengine ya mlipuko kikiwamo kipindupindu.

"Mbali na kuhimiza chanjo, tumehamasisha ununuaji wa ndoo na kuziweka pembeni mwa visima vya kuteka maji ili kila anayekuja kupata huduma hiyo, anawe kwanza kabla ya kushika kamba ya kutekea maji," alisema Biashagazi.

Mkurugenzi huyo alisema katika kampeni hiyo, zaidi ya ndoo 60 zimewekwa pembeni mwa visima vya maji ndani ya Kata ya Kipunguni na kwamba njia hiyo waliobuni inaweza kusaidia watu kuepusha watu kwa kuambikizwa ugonjwa huo na mengine.

Seleman alisema, kwa sasa ni lazima mtu anawe maji tiririka kwa sabuni na vitakasa mikono kabla hajashika kamba kuchota maji, kwa ajili ya usalama wa afya yake na ya wengine.

"Ikumbukwe kuwa mtu anatoka nyumbani kwake na huenda amepata maambukizi kwa kushika vitu ambavyo si salama au wakati mwingine ametoka chooni hajanawa vizuri, kisha anakwenda kisimani anashika kamba ya kuteka maji, anaweza kuambukiza wengine," alisema.

Alisema kutokana na mazingira hayo, wakaamua kushirikiana na maofisa afya wa Kata ya Kipunguni, wamiliki wa visima vya maji kuweka mkakati wa kununua ndoo za maji tiririka.

"Kuna wakati tulifanya utafiti mdogo tukabaini kuwa watu 94 huenda kuteka maji katika kisima komoja, sasa ikitokea kuna mtu ameshika kamba akiwa na hajanawa vizuri anaweza kuwaambukiza wote," alisema.

Mwanaharakati Epiphania Kamugisha, alisema hamasa kama hiyo kwa jamii ni ya muhimu ili kuhakikisha inapata uelewa kuhusu mbinu za kuepuka magonjwa mbalimbali ukiwamo ugonjwa wa UVIKO-19.

"Hatua zilizochukuliwa na Sauti ya Jamii Kipunguni za kuanzisha kampeni za kuwa na ndoo za maji tiririka pembeni mwa visima vya maji ni ya kuungwa mkono kwani zinasaidia watu kuwa salama," alisema Kamugisha.

# Maelfu wapata elimu ya bidhaa za viwango

**Na Mwandishi Wetu**

WANANCHI zaidi ya 15,000 katika Wilaya za Songwe, Njombe, Mufindi na Halmashauri ya Wilaya ya Iringa wamepatia elimu kuhusiana na umuhimu wa kununua bidhaa zilizothibitishwa na Shirika la Viwango Tanzania (TBS) sambamba na kuhamasisha wafanyabiashara kusajili maduka ya chakula na vipodozi.

Kampeni hiyo ya kutoa elimu kwa wanachi hao ilianza Mei 7, mwaka huu, katika wilaya hizo na kuhitimishwa mwanzoni mwa wiki hii, ambapo ilifanyika katika maeneo mbalimbali yakihusisha na shule za msingi na sekondari, masoko, stendi, minadani na maeneo mengine ya wazi ambapo wananchi walijitokeza kwa wingi kupata elimu na ufahamu wa masuala mbalimbali yahusuyo ubora wa bidhaa.

Akizungumzia kampeni hiyo Mkuu wa Idara ya Elimu Sekondari wa Halmashauri ya Mji wa Mafinga, Stephen Shemdoe, aliipongeza TBS kwa kutoa elimu kwa wanafunzi na alishauri kuanzishwa kwa klabu za kudumu za masuala ya viwango katika shule za sekondari kwa miaka ijayo ili elimu hiyo iwe endelevu.

Kwa upande wake Meneja Uhusiano na Masoko wa TBS, Gladness Kaseka, aliwakumbusha wananchi kutambua kuwa vita ya bidhaa hafifu sio ya TBS pekee, bali ni ya Taifa kwa ujumla.

"Katika kampeni hii tumeweza kuwafikia wananchi 15,865 kati yao wanafunzi wa shule za msingi na sekondari 9,144 na wananchi 6,721," alisema Kaseka.

Kaseka aliwafafanulia wanafunzi pamoja na walimu kuhusu umuhimu wa viwango katika maisha yao ya kila siku vile vile kuwafahamisha fursa ya huduma bure kwa wajasiriamali wadogo.

Aliwataka wananchi waliopata elimu hiyo kuhakikisha wanakuwa mabalozi kwa kuhamasisha ubora katika jamii wanazoishi.

Aidha, alitoa wito kwa wananchi kuendelea kutoa taarifa pindi wanapokutana na bidhaa zilizokwisha muda wake au wanapotilia shaka bidhaa yoyote katika soko.

Kwa upande wa wafanyabiashara aliwataka kuhakikisha wanafuatilia taratibu sahihi za usajili wa bidhaa au majengo ya chakula na vipodozi kwa kutembelea ofisi ya TBS iliyopo karibu au kupiga katika kituo cha huduma kupitia mawasiliano yaliyotolewa.

Kampeni ya kuelimisha umma inayotolewa na shirika hiyo ni endelevu itaendelea katika wilaya za mikoa ya kaskazini.

# Wanafunzi watakiwa kuzingatia malengo yao

**Na Christina Haule,**
MOROGORO

WANAFUNZI wa kike nchini wameaswa kusimamia na kuzingatia malengo yao, masomo na maisha ya baadaye, kwa kuacha kuingia kwenye mahusiano ya kimapenzi ambayo yanaweza kuwasababishia kupata ujauzito, ndoa za utotoni na magonjwa, jambo litakalokatiza ndoto zao.

Ofisa Ustawi wa Jamii Manispaa ya Morogoro, Joyce Mugambi, aliyasema hayo jana kwa niaba ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa, Ally Mchella, wakati wa ufunguzi wa kongamano la kugawa taulo za kike 200 kwa wanafunzi kutoka shule za sekondari 11 za Kata za Manispaa ya Morogoro lililoandaliwa na Taasisi ya Wezesha Mabadiliko (WEMA).

Alisema wakiwa wanafunzi wanapaswa kutofanya majukumu ya mama kwa kuhudumia wanaume huku wakisoma na kutakiwa kufanya mtihani jambo ambalo alidai hawataliweza bali wazingatie masomo huku wakiwa na nidhamu shuleni kwa sababu dunia ya sasa ni ya ushindani.

"Ni bora ukafaulu na kupata hata daraja la tatu au nne ya mwanzo kama umekosa la kwanza na pili, hiyo itakusaidia hata ukiamua kufanya biashara au vinginevyo sababu kwa sasa hata wanaume hawaoi mwanamke asiyesoma," alisema.

Awali Mkurugenzi wa WEMA, Dk. Lusako Mwakiluma, akitoa mada ya kujiamini aliwataka wanafunzi hao kuzingatia mbinu 10 za mafanikio ya maisha kwa muda mfupi na mrefu na kuacha kujiingiza kwenye vitendo vilivyo kinyume na maadili vitakavyopelekea kufanyiwa ukatili.

Alizitaja mbinu hizo kuwa ni kuandika malengo ya maisha, kuwa na nidhamu ya mambo, kuwa tayari kufanya walichopanga kufanya, kujali afya zao, kujali muda, kuwa na taarifa sahihi kwao na wengine, kuwa na marafiki sahihi, kusimama uelekeo walioanzisha na kujithamini, kujiamini na kujikubali.

Akizungumzia pedi za kufua zilizogawiwa kwa wanafunzi hao, Mkurugenzi huyo aliwaasa wanafunzi kuzingatia matumizi ya pedi hizo ambazo zinadumu ndani ya mwaka mmoja na miezi minane, ili ziwasaidie katika kuendeleza maisha yao ya usichana na masomo salama wawapo shuleni.

Naye Inspekta wa Polisi kutoka Dawati la Jinsia Jeshi la Polisi mkoani hapo, Mwanaidi Lwena, alisema wanajipanga kuanzisha klabu za jenda na masuala ya kupinga ukatili wa kijinsia katika shule 10 za Sekondari za kata Manispaa ya Morogoro.

Inspekta Lwena alisema ufunguzi wa klabu hizo utasaidia polisi kutoa elimu ya masuala ya ukatili wa kijinsia na jenda kwa wanafunzi sambamba na polisi kupata taarifa mbalimbali za wanafunzi wa kike, ikiwamo wanafunzi kutongozwa na walimu wa kiume na kukosa kwa kutoa taarifa ili wapate msaada sababu wasaidizi wenyewe kuwa wahusika wa masuala hayo.

Naye mmoja wa wanafunzi hao, Neema Matokeo mwanafunzi wa kidato cha tatu, Shule ya Sekondari Uwanja wa Taifa, alisema kundi hatarishi kwao ni wauza chipsi na waendesha pikipiki maarufu kama bodaboda, wanaowalaghai kiasi cha baadhi kuingia kwenye mahusiano.




Meneja Raslimali Watu wa Mgodi wa Bulyanhulu, Lumbu Kambula, akiongea katika kongamano la kuwajengea uwezo wanafunzi wa vyuo vikuu nchini lililoandaliwa na Taasisi ya AIESEC Tanzania, lililofanyika Chuo Kikuu cha Dodoma kwa udhamini wa kampuni ya Madini ya Barrick. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# 50 wanusurika kifo basi likipinduka

**Na Gideon Mwakanosya,**
SONGEA

ZAIDI ya abiria 50 waliokuwa wakisafiri kutoka Songea kwenda Dar es Salaam kupitia njia ya Lindi wamenusurika kufa baada ya basi la Superfeo walilokuwa wakisafiria kuacha njia na kupinduka.

Habari zilizopatikana jana na kuthibitishwa na Mkuu wa Wilaya ya Tunduru, Julius Mtatiro, zilisema kuwa ajali hiyo ilitokea katika kijiji cha Huria barabara ya Songea kwenda Tunduru majira ya saa 3.00 asubuhi.

Ajali hiyo inahusisha gari aina ya Scania yenye namba za usajili T694 DXF mali ya kampuni ya Superfeo yenye makao makuu Manispaa ya Songea, mkoani Ruvuma iliyokuwa ikiendeshwa na Halima Mbwana, ambaye inadaiwa amekatika mkono wa kulia katika ajali hiyo.

Alifafanua kuwa katika ajali hiyo kulikuwa na abiria zaidi ya 50 ambao walikuwa wakielekea Dar es Salaam na baadhi ya abiria wamejeruhiwa na kukimbizwa katika Hospitali ya Misheni ya Kiuma kwa matibabu zaidi.

Mtatiro alisema ajali hiyo imesababisha majeruhi 19 na hakuna kifo, kati yao 14 walipatiwa matibabu na kuruhusiwa na wengine waanendelea kupatiwa matibabu huku baadhi wakitarajiwa kupewa rufani kwenda hospitali kubwa kwa matibabu zaidi.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Ruvuma, Joseph Konyo, akiongea na Nipashe kwa njia ya simu alithibitisha kutokea kwa ajali hiyo.

# Serikali yafafanua vigezo fedha za Mfuko wa Jimbo

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Dk. Selemani Jafo, ametaja vigezo vinne vinavyotumika kugawa fedha za kuchocheo maendeleo ya jimbo.

Dk. Jafo aliyasema hayo jana bungeni alipojibu swali la Mbunge wa Malindi (CCM), Mohamed Suleiman Omar, aliyetaka kujua mpango wa serikali wa kupitia upya fedha za mfuko wa kuchocheo maendeleo ya jimbo na kuongeza fedha kwa upande wa Zanzibar.

Akijibu swali hilo, Waziri Jafo alisema kifungu cha 5(3) cha Sheria ya Mfuko wa Jimbo kimefafanua vigezo vinavyotumika kugawa fedha hizo.

Alitaja vigezo hivyo kuwa ni mgawo sawa kwa kila jimbo asilimia 25, idadi ya watu asilimia 45, kiwango cha umaskini asilimia 20 na ukubwa wa eneo asilimia 10.

"Serikali itaendelea kuangalia uwezekano wa kuboresha mgawo wa fedha za Zanzibar kulingana na upatikanaji wa mapato," alisema.

Mbunge wa Lulindi (CCM), Issa Mchungahela, alihoji kama fedha za mfuko huo zinapaswa kutumika kununulia samani za Ofisi ya Jimbo.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), David Silinde, alisema mfuko huo ulianzishwa kwa sheria namba 16 ya mwaka 2009.

"Fedha za Mfuko wa Jimbo ni mahususi kwa ajili ya kutekeleza miradi ya kijamii iliyoanzishwa na wananchi wa jimbo husika," alisema.

Silinde alisema halmashauri zilielekezwa kuwapatia wabunge ofisi kwa ajili ya shughuli zao ikiwa ni pamoja na samani kulingana na uwezo wao wa ukusanyaji mapato yao ya ndani.

"Ninachukua fursa hii kuwasihi wakurugenzi wa halmashauri kushirikiana na wabunge katika kutekeleza majukumu yao," alisema.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais, Selemani Jafo, akijibu maswali yaliyoulizwa na baadhi ya wabunge kwenye mkutano wa Bunge wa saba kikao cha 28 jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Waonywa uvamizi mazalia ya samaki

WIZARA ya Mifugo na Uvuvi, imesema haitasita kuchukua hatua kwa mtu yeyote atakayeingia kwenye eneo lililotengwa kwa ajili ya mazalia ya samaki.

Naibu Waziri wa Wizara hiyo, Abdallah Ulega, aliyaeleza hayo bungeni jana alipojibu swali la nyongeza la Mbunge wa Nkasi Kaskazini (CHADEMA), Aida Khenani, aliyetaka serikali kuweka mkakati wa ziada wa kulinda mazalia ya samaki bila kuathiri wavuvi.

Akijibu swali hilo, Ulega alisema|; "Huo ni uhalifu na hatutamvumilia yeyote atakayekwenda kuharibu rasilimali hii ya Watanzania, bila kulinda mazalia ya samaki watapotea."

Alisema serikali kwa kushirikiana na jamii imejipanga kuyatambua, kuyaainisha na kuyatangaza kwa mujibu wa sheria ili yalindwe.

Katika swali la msingi, mbunge huyo alihoji mpango wa serikali kujenga soko la kisasa la mazao yatokanayo na uvuvi wilayani Nkasi.

Ulega, akijibu swali hilo, alisema mpango wa serikali ni kujenga na kuboresha miundombinu ya uvuvi ikiwamo mialo na masoko katika maeneo mbalimbali nchini.

"Kwa upande wa mwambao wa Ziwa Tanganyika unaojumuisha Wilaya ya Nkasi, shughuli za uvuvi zinafanyika katika mialo ipatayo 239," alisema.

Kati ya mialo hiyo, alisema serikali imeboresha mialo minne ya Kibirizi (Manispaa ya Kigoma ujiji), Ikola (Tanganyika), Muyobozi (Uvinza) na Wilaya ya Kirando (Nkasi).

Alisema serikali imejenga na kuboresha masoko mawili ya samaki ya Kibirizi (Kigoma) na Kasanga (Sumbawanga).

"Pia, kwa sasa serikali inaendelea na jitihada za kuupandisha hadhi mwalo wa Kirando ulioko Wilaya ya Nkasi ili ufikie hadhi ya kuwa soko la kisasa la samaki na mazao ya uvuvi," alisema.

## Wilaya zote kufikiwa mkongo wa taifa 2025

NAIBU Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Andrea Kundo, amesema wilaya zote nchini zitafikiwa na huduma za mkongo wa taifa wa mawasiliano ifikapo mwaka 2025.

Alitoa kauli hiyo bungeni jana alipojibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Amina Ali Mzee, aliyehoji ni lini serikali itapeleka mkongo wa mawasiliano wa taifa katika wilaya 14 ambazo hazijafikiwa ikiwamo Mjini Magharibi na Kusini Unguja ili kurahisisha utoaji huduma kwa wananchi.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Kundo alisema serikali kupitia Wakala wa Miundombinu ya Mawasiliano Zanzibar (ZICTIA) imefikisha huduma za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano katika mikoa na wilaya zote za Zanzibar.

"Mjini Magharibi inapata huduma kupitia vituo vilivyoko maeneo ya Jamhuri Garden, Fumba na Ofisi za ZICTIA na Kusini Unguja inapata huduma kupitia kituo kilichopo Paje," alisema.

Alibainisha kuwa hadi sasa jumla ya wilaya 43 nchini zimefikiwa na mkongo wa mawasiliano wa taifa.

"Kwa bajeti ya mwaka wa fedha 2021/2022 jumla ya wilaya mpya 23 zitafikiwa na hivyo kuwa na jumla ya wilaya 66 nchini zenye huduma ya mkongo wa taifa wa mawasiliano," alisema.

Naibu Waziri alisema kwa mwaka wa fedha 2022/23 wilaya zingine mpya 15 zitafikiwa na hivyo kuwa na jumla ya wilaya 81.

## Serikali yasaka fedha skimu za umwagiliaji

SERIKALI imesema inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kukamilisha skimu zote za umwagiliaji nchini ikiwamo ya Ifumbo wilayani Chunya.

Naibu Waziri wa Kilimo, Anthony Mavunde, alitoa kauli hiyo jana bungeni alipojibu swali la Mbunge wa Lupa (CCM), Masache Kasaka.

Mbunge huyo alihoji ni lini serikali itatoa fedha ili kukamilisha ujenzi wa Skimu ya Umwagiliaji katika Kata ya Ifumbo, Chunya, akibainisha mradi huo ulianza mwaka 2006.

Alihoji mkakati wa serikali wa kutumia Bonde la Mto Lupa kwa kuwa unafaa kwa kilimo cha umwagiliaji.

Akijibu maswali hayo, Naibu Waziri Mavunde alisema serikali inatambua umuhimu wa skimu ya umwagiliaji ya Ifumbo yenye eneo la hekta 250, kulimwa mazao ya mpunga, alizeti, ufuta, mboga na mahindi kwa wananchi wa Chunya.

"Kwa kutambua umuhimu wa skimu hiyo, serikali ilitenga kiasi cha Sh. milioni 400 kupitia Programu ya Kuendeleza Kilimo (ASDP I) na Sh. milioni 50.58 kupitia Programu ya Kuendeleza Kilimo Wilayani (DADPs) katika mwaka wa fedha 2008/2009.

"Fedha hizo zilitumika kujenga miundombinu ya umwagiliaji ikiwamo banio, vigawa maji 11, vivuko vya miguu 10 na mfereji mkuu wenye urefu wa mita 2,165," alisema.

Mavunde alisema serikali inatambua umuhimu wa kilimo cha umwagiliaji nchini na hasa ukizingatia mabadiliko ya tabianchi yanayosababisha mtawanyiko wa mvua isiyotabirika.

Hata hivyo, alisema wiki hii wizara itatuma timu ya Tume ya Umwagiliaji kwenda kupitia Bonde la Mto Lupa ili kushauri.


Ukurasa 12

TEHAMA inavyookoa muda TBS






Ukurasa 13

**Kushusha umeme, vifaa vya kupikia kutakavyomaliza uhaba wa nishati mijini**

Nipashe
TESA
Jumanne Mei 24, 2022
TEKNOLOJIA · ELIMU · SAYANSI

TEKNOLOJIA
NA GAUDENSIA MNGUMI

# Ufahamu ugonjwa wa mahindi unaotibika kwa kupima DNA



Mahindi yaliyoharibiwa na viwavijeshi vamizi. **PICHA: MTANDAO**

KILIMO cha mahindi kinawatoa machozi wakulima karibu kote nchini kutokana na ugonjwa wa 'fall army waves' au viwavi vamizi unaoshambulia mahindi wiki chache baada ya kuota.

Maradhi haya huletwa na viwavijeshi vamizi, wanaovamia mahindi muda mfupi baada ya mbegu kuota vikila majani, kutafuna shina, maua (mbelewe), maganda, nyuzi, gunzi na punje za mahindi.

Yote hayo yamezalisha malalamiko na hisia nyingi kuhusu ugonjwa huo ambao wengine wanadai hautibiki, umetengenezwa na kampuni za ng'ambo zinazozalisha mbegu na unapoingia ardhini (shambani) hauishi hata ukichoma udongo huwezi kuumaliza. Pamoja na ugali Watanzania huandaa milo mbalimbali inayotokana na mahindi kama kande, 'makukuru' gidheri, loshoro na pia pombe za asili hutengenezwa kwa mahindi.

Nipashe inazungumza na mtafiti mbobezi wa magonjwa ya mazao Dk. Joseph Ndunguru ambaye ni Mkurugenzi wa Kituo cha Utafiti Mikocheni (TARI-Mikocheni), jijini Dar es Salaam, kuhusu madai hayo ya wakulima, ugonjwa na mikakati ya udhibiti.

***SWALI:*** Tufahamishe kuhusu ugonjwa mpya wa viwavi vamizi unaoshambulia mahindi

***JIBU:*** Unatokana na 'larva' au viwavi wanaoeneza ugonjwa huu wa mahindi ambao leo unaonekana karibu kila kwenye mashamba ya mahindi. Hautokani na mbegu wala hauishi ardhini ni mgeni hauna asili ya Tanzania umetokea ng'ambo na vimelea vimefika nchini kupitia shughuli mbalimbali za usafirishaji na ubebaji watu na bidhaa. Vimelea huishi angani.

Viwavijeshi vamizi vina asili ya Amerika na hapa kwetu viliingia 2017 katika mikoa ya kaskazini, vikitokea Kenya na Ethiopia na vimesambaa sehemu kubwa. Lakini si nchini tu, ni Afrika karibu yote panapolimwa mahindi. Nchi nyingi za Kusini ya Jangwa la Sahara na Afrika Kusini zimeathirika.

"Viwavi vinaharibu mahindi katika hatua zote vinakula magunzi, majani, maganda, punje na shina, mmea ukiwa shambani."

Changamoto kubwa waliyonayo wakulima ni kununua viuatilifu ambavyo vinaweza kudhibiti au visidhibiti viwavi kulingana na hatua za ukuaji na jamii ya wadudu hao.

"Utafiti uliofanyika TARI Mikocheni unaonyesha kuwa licha ya kulingana na kufanana viwavi hawa unapowatazama kwa macho, ukweli ni kwamba wapo jamii nyingi sana, tena wanatofautiana mno".

Ukweli unajulikana kwa kufanya kipimo cha nasaba -DNA kinachobainisha tabia za kibailojia, maumbile yao na utofauti wa kila kiwavi ili kwamba tuandae au kutambua dawa za kudhibiti kwa kutumia viuatilifu tofauti kulingana na makundi tunayoshughulika nayo.

"Ndiyo maana kabla ya kutoa dawa ni lazima kupima kwanza DNA zao. Kwa sababu viwavijeshi vilivyoko Tabora ni tofauti na vinavyopatikana Sengerema, Songea au Mbeya. 'Genetic groups' (makundi ya kimaumbile) ni tofauti na vinaweza kudhibitiwa kwa viuatilifu tofauti na si aina moja. Ili kuwa na udhibiti endelevu kitu cha kwanza lazima kupima DNA ili tujue ni mdudu wa aina gani tunayeshughulika naye na anadhibitika na dawa ipi."

Ili kuwa na udhibiti endelevu ni lazima kujua ni aina gani ya mdudu au kiwavi vamizi tunachoshughulika nacho kipo mkoa fulani kutegemeana na nasaba-DNA zake.

Hii itawezesha kufikisha viuatilifu sahihi eneo sahihi kutibu wadudu sahihi ili kuwa na udhibiti endelevu, hivyo kazi ianze na kupima sampli za DNA za wadudu hao kwenye mashamba ili kufahamu aina zao na dawa muafaka.

Jambo la muhimu ni kwa kupima DNA kwa kila eneo na kutengeneza ramani ya kila mkoa yenye maelezo na aina ya wadudu na kusambaza dawa kwa kila mkoa kulingana na viwavijeshi walioko eneo hilo."

Ni kwasababu japo wanafanana lakini siyo jamii moja hivyo hawawezi kutibiwa na dawa za aina moja siyo kama malaria, ndiyo maana uchunguzi wa DNA ni jambo la muhimu kabla ya kudhibiti.

"Lazima kujua aina ipi inapatikana wapi ili tuweze kujua njia bora na endelevu za kuwadhibiti na tunaposambaza viuatilifu ile ramaniya taifa ituongoze mfano Mbeya tupeleke jamii hii na Kagera au Arusha aina nyingine ya dawa."

***SWALI:*** Vipi kuhusu madai kuwa wadudu hawasikii dawa au ni sugu, DNA imebaini hilo?

***JIBU:*** Bila kupima DNA na kuzijua tunaweza kuchukua viuatilifu kwa ajili ya kudhibiti aina hii tukavipeleka kwa wadudu ambao dawa hiyo si muafaka kwao, hivyo

**INAENDELEA UK.14**

TEKNOLOJIA NA SABATO KASIKA

# TEHAMA inavyookoa muda TBS

## • Mtoa huduma, mteja hawaonani

KATIKA juhudi za kuboresha huduma zake, Shirika la Viwango Tanzania (TBS) limegeukia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), ili kuondoa urasimu usio wa lazima, kupoteza muda likilenga kuhudumi umma kwa tija.

Shirika hilo limeanzisha mfumo wa utoaji huduma kwa njia ya mtandao Online Application System' (OAS), unaopatikana na kwenye mtandao duniani kote kwa tovuti ya http://oas.tbs.go.tz.

Meneja wa TEHAMA wa TBS, Jabir Abdi, anatoa maelezo hayo wakati wa kutoa taarifa za kazi za BS kwa wana habari, akieleza kuwa mfumo huo utaokoa muda wa mteja, kwa kuwa hawezi kufika ofisi za shirika hilo kupata huduma, kwa madai kwamba, zinapatikana popote alipo.

Aidha, anasema, OAS inadhibiti mianya ya rushwa, kwa kuwa muomba huduma na mhudumu hawaonani na pia mrundikano wa mafaili ya maombi na muda wa kumhudumia mteja vimepunguzwa.

"Ndani ya siku tatu mteja anapata huduma na inawezekana anahudumiwa ndani ya siku moja au mbili, lakini haiwezi kuzidi tatu, kwani ndani ya siku hizo anatakiwa awe amehudumiwa," anasema Abdi.

Meneja huyo anafafanua kuwa kwa kupitia mifumo ya njia ya mtandao ya TBS, wafanyabiashara wanapata orodha za bidhaa zinazotakiwa kukaguliwa nchini, na kwamba huduma yote inapatikana kupitia OAS.

### MWANZO NI MGUMU

Anasema kulikuwapo na changamoto hasa kutokana na baadhi ya wateja kutolewa jinsi ya kutumia mfumo huo wa TEHAMA, na kwamba shirika lilitoa mafunzo kwa wale ambao walikuwa hawajauelewa.

"Wajasiriamali ambao bado wako nyuma katika matumizi ya TEHAMA, tunaendelea kuwapa elimu endelevu, kwani mjasiriamali popote alipo anaweza kupiga simu anaelekezwa jinsi kutunia mfumo huo," anasema.

Anaongeza kuwa katika ofisi za TBS za kanda kama kuna mjasiriamali ana shida katika matumizi ya mfumo huo, wanampa mafunzo na maelekezo mbalimbali njia ya simu na kwamba hatua hiyo imekuwa na mafanikio.

"Hadi sasa hatujapata malalamiko, hiyo inaonyesha kwua elimu tunayotoa imewasaidia, kwani wanapata huduma kwa wakati, hivyo si lazima mteja afike ofisini kupata huduma bali anahudumiwa huko huko aliko," anasema.



Wataalamu wa maabara wa TBS wakiwa kazini. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

> TBS ina majukumu ya kutayarisha na kusimamia viwango vyote vya kitaifa, kutoa ushauri viwandani juu ya uzalishaji wa bidhaa bora, kupima na kuhakiki vipimo vinavyotumika viwandani.



### KUSAMBAZA MAABARA

Meneja Upimaji wa shirika hilo, Joseph Makene, anasema TBS ina maabara tisa zinazotumika kuchunguza bidhaa mbalimbali ambazo ni bora na vifaa vya kisasa vya uchunguzi na wataalamu waliobobea katika uchunguzi.

Akitoa taarifa kuhusu kazi za maabara hizo zilizopo makao makuu ya TBS, Ubungo Dar es Salaam, anafafanua kuwa kuna maabara za uchunguzi wa bidhaa zote.

"TBS tuna maabara za kupima nguo na ngozi, zinatumika kuchunguza bidhaa zote zinazohusu nguo na ngozi pia zipo kupima vifaa vya kikemikali ambayo hutumika kupima vipodozi na bidhaa zote za petroli," anasema Makene.

Anaongeza kuwa shirika hilo pia lina maabara tatu za uhandisi ikiwamo ya uhandisi umeme ambayo inafanya uchunguzi wa vifaa vyote vinavyohusiana na umeme kama vile Tv, simu, kompyuta na vingine vingi.

"Lakini tuna maabara ya uhandisi mitambo ambayo inafanya uchunguzi wa bidhaa zote zinazohusu mitambo na pia ipo maabara ya ujenzi inayopima bidhaa zote za ujenzi kama mabomba yanayotumika katika kupitisha maji majumbani na kwenye miradi mbalimbali," anasema.

Makene anaitaja pia maabara nyingine za kupima vifungashio na ugezi ambayo inafanya ugezi wa vipimo vyote, ambavyo vinatumika katika uzalishaji viwandani na kwenye hospitali.

Aidha, anasema kwa sasa shirika hilo mbioni kusimika mitambo ya maabara kwenye kanda zake kwenye baadhi ya mikoani, ikiwa ni njia mojawapo ya TBS ya kusogeza huduma za upimaji karibu na wananchi.

Kwa mujibu wa Makene, kanda hizo ni Mwanza, Kigoma, Dodoma, Mtwara, Mbeya, Arusha, huku akitoa wito kwa wazalishaji wa bidhaa kutumia TBS kuthibitisha ubora wa bidhaa zao.

"Ninatoa wito huu kwa wale ambao hawana maabara, kwani tunajua wapo wengine tayari wana maabara zao wanataka kutengeneza vitu vyenye ubora unaokubalika, lakini wasiokuwa na maabara watumie za TBS," anasema.

### FAIDA ZA VIWANGO

Meneja Viwango wa shirika hilo, Yona Afrika anasema, viwango vina faida nyingi, ikiwamo kuweka usawa katika uwanja wa biashara, kuondoa mkanganyiko kuhusu bidhaa pia husaidia kufungua masoko zaidi.

"Viwango hurahisisha biashara kati ya nchi na nchi, vinahakikisha wa ubora, usalama, kuaminika, ufanisi na huipa serikali urahisi wa kuunda sheria za masuala ya afya na usalama wa watumiaji wa bidhaa," anasema Afrika.

Akielezea utayarishaji wa viwango, Afrika anasema hutayarishwa kwa kuleta pamoja pande zote zenye maslahi kuanzia wazalishaji, watumiaji na wasanifu katika kila kifaa, bidhaa, mchakato au huduma.

"TBS ina majukumu ya kutayarisha na kusimamia viwango vyote vya kitaifa, kutoa ushauri viwandani juu ya uzalishaji wa bidhaa bora, kupima na kuhakiki vipimo vinavyotumika viwandani," anasema.

Anataja baadhi ya majukumu mengine kutoa mafunzo kwa wafanyakazi wa viwandani, udhibiti wa bidhaa zenye ubora hafifu, utoaji wa alama na cheti cha ubora wa bidhaa za ndani na nje ya nchi.

"Lakini pia tunaelimisha umma juu ya masuala yote yanayohusu uwekaji na usimamizi wa viwango na udhibiti ubora wa bidhaa viwandani na usajili wa chakula na vipodozi," anasema.

ELIMU

NA DK. FELICIAN KILAHAMA

# Kushusha bei umeme, vifaa kupikia kutakavyomaliza uhaba wa nishati

KWANZA nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa zawadi ya uhai na afya njema maana ndiye mwenye hatimiliki ya uhai wetu. Kadhalika, namshukuru kwa kuijalia Tanzania rasilimali nyingi za asili kama misitu na wanyamapori.

Mwaka 2021 taifa limefikisha miaka 60 ya Uhuru uliopatikana Desemba 9, 1961 ni kipindi kirefu sawa na binadamu aliyezaliwa, akakua na akafikisha umri wa kuitwa mzee au raia mwandamizi.

Kwa hiyo ni dhahiri 'raia Tanzania' amepitia na kushuhudia mengi katika safari ya maisha yake.

Wakati wa uhuru karibu nchi nzima ilikuwa imefunikwa na misitu ya asili hususani aina ya "miyombo" na kwenye milima ya Kilimanjaro na Meru pamoja na milima katika Tao la Mashariki, Milima ya Livingstone na Rungwe, ilikuwa ni Tanzania ya kijani iliyojaa misitu minene ya kitropiki.

Tanzania ilibahatika kuwa na urithi wa aina hiyo ya misitu pamoja na maliasili nyingine ikiwamo ardhi ya kutosha. Rasilimali misitu ni tegemeo kwa Watanzania walio wengi kumudu maisha ya kila siku.

Karibu kila familia au kaya, kwa namna moja au nyingine, inatumia huduma na bidhaa za misitu. Tangu uhuru hadi sasa rasilimali misitu imekuwa chanzo muhimu cha kuni, mkaa, dawa asilia, chakula mfano, matundapori, wadudu waliwao, uyoga, mboga asilia, wanyamapori, asali, maji na kupata nguzo, fito na mbao.

Vilevile, kupata malighafi za kutengeneza mikeka, nyungo na vikapu. Isitoshe kufuatana na ongezeko la watu chini ya milioni 10 wakati wa uhuru na sasa zaidi ya milioni 50 ni dhahiri mahitaji na matumizi ya rasilimali misitu yamekuwa yakiongezeka sana.



Jiko la umeme lenye presha 'electric pressure cooker' linapika kwa ufanisi kwa kutumia umeme kidogo, hivyo kuwa mbadala wa mkaa. **PICHA: MTANDAO**

### KILIO NISHATI KUPIKIA

Wengi wanaoishi mijini wanatumia zaidi mkaa na kuni kupikia wakati vijijini kuni zinatumika zaidi.

Kwa miaka ya karibuni tumeshuhudia changamoto nyingi kuhusu upatikanaji wa nishati ya kupikia sehemu za mijini. Vipo vyanzo kadhaa vya nishati mijini, gesi mfano, biogas, gesiasilia, au itokanayo na mafuta ( LPG), umeme, umeme jua (solar), kuni, mkaa (wa miti unaotokana na tungamotaka (briquettes), lakini kwa mijini wengi wanatumia mkaa wa kawaida ingawa kwa miaka kama mitano iliyopita pia gesi ya LPG inatumika na wachache wameunganishwa na gesiasilia.

Matumizi mchanganyiko wa nishati hizi kupikia yalilenga kupunguza utegemezi mkubwa kwa mkaa. Hata hivyo, kwa miaka kadhaa hali imekuwa ikibadilika haraka na wengi kuendelea kutumia mkaa zaidi kuliko vyanzo vingine.

Kwa sasa bei za nishati ya kupikia zilikuwa changamoto sana. Siyo mkaa, gesi, wala umeme na inaweza kusema kuna unafuu kutokana na bei zake kuendelea kupanda.

Karibu kila kona malalamiko ni 'gharama za maisha' kutokana na bei kupanda mara kwa mara. Mkaa uliokuwa unatumiwa na wengi sasa hali imekuwa siyo ya kuridhisha kutokana na upatikanaji wake lakini bei kupanda.

Katika mahojiano yaliyofanyika Kimara jijini Dar es Salaam na wauzaji na watumiaji wa mkaa wanasema wanatumia karibu Shilingi 3,000 kununua mkaa wa siku takriban Shilingi 90,000 kwa mwezi, lakini wakitumia gesi ya kilo15 kwa mwezi inayonunuliwa kati ya Shilingi 53 hadi 60.

Je, hali kwa wengi wa kipato cha chini inakuwaje, wakiwamo wanaolipa kodi ya nyumba na kununua chakula na mahitaji mengine muhimu kama dawa? Anahoji mama mmoja akisema "mkaa wa siku hizi pia haukai, unaisha haraka kwa sababu unatokana na miti inayokatwa kabla haijakomaa," akisema hiyo nayo ni changamoto kwa mazingira nchini.

Matumizi ya gesi na umeme ni kilio kutokana na gharama kuwa kubwa sana kwa vyanzo hivyo vya nishati pia vifaa kama 'pressure cookers' au 'rice cooker', au majiko ya gesi na umeme bei zake ni kubwa.

Mathalani, 'rice cooker' bei yake inaanzia Shilingi 100,000 wakati jiko lenye umeme na gesi kwa pamoja majiko matatu gesi na sehemu moja umeme bei yake ni zaidi ya shilingi 600,000.

Isitoshe mafuta ya taa yamepanda bei lita moja ni zaidi ya Shilingi 3,000 kiasi kwamba ni shida wengi kuyatumia. Kuendelea kutumia mkaa na kuni kwa wingi pia ni tishio kwa misitu na mazingira ikiwamo kuhatarisha uhai wa wanyamapori.

### MAPENDEKEZO SERIKALINI

Takwimu zinaonyesha kuwa kila mwaka Tanzania inapoteza hekta kati ya 370,000 na 470,000 za misitu kasi ya ukataji miti ni kubwa katika mikoa ya magharibi (Katavi, Kigoma, Rukwa na Tabora) ukilinganisha na mikoa mingine.

> Mathalani, 'rice cooker' bei yake inaanzia Shilingi 100,000 wakati jiko lenye umeme na gesi kwa pamoja majiko matatu gesi na sehemu moja umeme bei yake ni zaidi ya shilingi 600,000.

Ikiwa kuni na mkaa ni vyanzo muhimu vya nishati ya kupikia, je, Wizara ya Nishati ina mipango gani kuhakikisha Watanzania wanapata nishati hiyo bila kuhatarisha mazingira?

Suala la nishati ya kupikia linachukuliwaje? Inatengewa fedha kama ilivyo kwa vyanzo vingine vya nishati nchini, umeme, gesi, mafuta? Iwapo serikali imetoa Shilingi bilioni 100 kufidia gharama za mafuta, ni vizuri pia ikaangalia uwezekano wa kufanya hivyo kufidia gharama za vyanzo vya nishati ya

kupikia ikiwa ni pamoja na kufidia bei za vifaa vya kupikia vya gesi na umeme. vilevile, kupunguza bei ya gesi na umeme ili vyanzo hivyo vitumike zaidi kupikia kuliko kutegemea sana mkaa na kuni.

Matumizi ya 'pressure rice cooker' vanaweza kuongezeka iwapo bei za vifaa hivyo zinashuka pamoja na bei za gesi yenyewe na umeme zinapungua ili kuleta unafuu wa maisha kwa watumiaji.

Wizara ya Nishati ikitenga bajeti ambayo itaweza kutoa auweni (ruzuku) kuwezesha wengi kutumia nishati hizo, mahitaji ya mkaa yatapungua hivyo kuchangia misitu ya asili kubaki salaam na kuhifadhi mazingira.

Hali hiyo italiwezesha taifa kupata mvua za kutosha, kupunguza mmomonyoko wa udongo (unaosombwa na maji ya mvua hadi kujaa kwenye mito), kutunza vyanzo vya maji na kuchangia katika kupunguza gesi ukaa ($CO_2$) angani hivyo kudhibiti mabadiliko ya tabianchi.

Hakuna lisilowezekana ni kwa serikali na wadau wengine kuliona hili na kuchukua hatua kwa manufaa ya wote.

Wakati huo, Wakala wa Huduma za Misitu (TFS) ukawezeshwa zaidi, pamoja na juhudi za kupanda miti, ili kusimamia misitu ya asili na kuhakikisha ukataji miti ovyo unadhibitwa ipasavyo.

Mkaa utokane na miti iliyosimamiwa isiwe kinyume chake. Chakula cha kutosha kitapatikana kutokana na mvua kunyesha kwa wakati na ardhi kuhifadhiwa vizuri na mabadiliko ya tabianchi yatadhibitiwa, mbuga za wanyama zitaimarika, ikiwamo wanyama kupata chakula na maji ya kutoisha.

Hali hiyo, itachochea zaidi utalii nchini na matunda ya 'Royal Tour' kushuhudiwa kitaifa na kwa wananchi wengi.

# Ufahamu ugonjwa wa mahindi unaotibika kwa kupima DNA

INATOKA UK.11

visimalize tatizo tukaendelea kulalamika kuwa ni dawa feki au viuatilifu sugu au wadudu hawadhibitiki.

Dawa hazifanyi vizuri kwa baadhi ya maeneo kutokana na kupeleka aina ambayo siyo ya kudhibiti viwavi hao. Ikumbukwe dawa hizi zinaagizwa ng'ambo lakini zinafanya vizuri kulingana na aina ya mdudu siyo wote.

"Hili tulijue tuchunguze kwanza tutambue kundi la wadudu ili kupeleka dawa inayostahili kwa udhibiti endelevu..."

***SWALI:*** Kipimo hicho kinapatikana nchini?

***JIBU:*** Teknolojia ya kupima DNA za viwavi hao na virusi vingine tunazo. Hii ilizinduliwa kwa mara ya kwanza duniani mkoani Mara. Tumeigundua wenyewe hapa TARI Mikocheni na hiki kipimo kinatoa majibu papo hapo shambani wala huhitaji kwenda maabara au kusafirisha sampuli.

Ni kipimo kidogo kinakunjwa kama 'stepla' unaweza kutembea nacho popote unafanya kila kitu shambani. Na gharama yake ni ndogo mkulima anayoimudu.

***SWALI:*** Kinaitwaje?

***JIBU:*** Kinajulikana kama 'Nano pore DN sequencer' tunachukua sampuli ya mimea tunapima na kupata majibu papo hapo na kutambua jamii ya dawa muda huo huo. Huu ndiyo mwarobaini wa kila kitu kwenye magonjwa kuanzia viwavi vya mahindi, virusi vya mihogo batobato na kantangaze inayoshambulia nyanya.



Viwavi jeshi vamizi vinavyoharibu mahindi tiba yake inapatikana kwa kupima DNA. **PICHA: MTANDAO**

***SWALI:*** Kama kuna teknolojia ipo, mbona inakuwa vigumu kuudhibiti?

***JIBU:*** Mipango ipo kwanza ni kuwahamasisha wadau wote wanaoshughulika na kilimo ili tuwe na uelewa wa pamoja kama taifa wa masuala ya wadudu hawa na viuatilifu vyake.

Tuhamasishane, kuanzia taasisi za udhibiti mfano Tasisi ya Kudhibiti Viuatilifu (TPRI), Taasisi ya Udhibiti wa Ubora wa Mbegu (TOSC), wanaoagiza pembejeo, watafiti, maofisa ugani, vikundi vya wakulima, asasi za kiraia (NGOS), wanahabari na viongozi wa vijiji ili tuwe na uelewa endelevu na udhibiti wa wadudu waharibifu wa mazao.

Tukisha kuwa na uelewa wa pamoja kila kundi linafanya jukumu lake, lakini tutakapokwenda kuagiza viuatilifu sahihi halifu vitatumika mahala sahihi, mfano dawa za Tanga, Iringa, Mbeya na Ruvuma.

Isiwe ni majaribio kama ilivyo sasa wakulima wametumia jamii nyingi za viautilifu, tena wauza pembejeo wanawaambia kajaribu hii ikishindikana urudi yote hayo ni hasara kwa mkulima, athari za kiafya kwa wananchi na uharibifu wa mazingira kuanzia maji, mimea na viumbe hai.

Hiki ndicho tunachofanya kuitoa sayansi kwenye maabara na kupeleka kwa wakulima mashambani ili ilete matokeo chanya na kubadilisha maisha ya wakulima.

Tutafanya maandalizi kuwa na mkakati na programu kitaifa ya kubaini DNA za viwavi vamizi inayoonyesha mtawanyiko wa viavi hivyo kote nchini. Ili kufanya utafiti huo tunatakiwa kuwa na rasilimali fedha, wataalamu na vietendea kazi vya kufanikisha programu hiyo.

***SWALI:*** Wakati mkijiandaa na mpango mkakati huo wa kitaifa wa kupima DNA na kusambaza viuatilifu sahihi unashauri wakulima na maofisa ugani wafanya nini?

***JIBU:*** Kwanza ni jukumu la viongozi wa serikali za mitaa kwa sababu wakulima wako kwenye eneo lao waanzae kuwahamasisha ili kuwakutanisha na wadau ili kuandaa mkakati wa udhibiti endelevu wa viwavijeshi vamizi.

La pili ni kutoa mafunzo kwa wakulima na maofisa ugani kuhusu matumizi sahihi ya viuatilifu sahihi vilivyoko na kuepusha matumizi mabaya ya dawa hizo yanayoendelea sasa.

***SWALI:*** Unazungumziaje kuhusu hasara inayotokana na kushambuliwa kwa mahindi hasa kwa wakulima wa Tanzania?

***JIBU:*** Hasara ni kubwa kumbuka asilimia 60 ya ardhi ya kilimo inayofaa kwa kilimo ipo Afrika, watu takribani milioni 800 wanategemea kilimo Afrika na kinaajiri takribani asilimia 55 ya Waafrika.

Mchango kwa pato la taifa kutoka kwenye sekta ya kilimo kwa nchi za Kusini ya Jangwa la Sahara ni asilimia 15 kwa sababu ya tija ndogo inayotokana na kukosekana maradhi ya kuongeza thamini, uzalishaji duni umechangiwa na kuwapo kwa magonjwa na wadudu waharibifu wa mazao.

Hasara inayotokana na mahindi kushambuliwa na viwavi kupotea tani milioni 8.5 mpaka milioni 16 za mahindi kila mwaka. Hiyo ni katika nchi 12 zinazozalisha mahindi kwa wingi barani Afrika kwa mujibu wa ripoti ya 'Taasisi ya Centre for Agriculture and Bioscience International' (CABI) ya mwaka 2016, na hasara yake ni takribani Dola bilioni 2.48 kwa mwaka.

## WANENAVYO MALENGA

### SENSA – BAJETI YAKE CHANGIA

Sensa ni jambo muhimu, kuifanya kumetimu,
Tunaifanya kwa zamu, ili kupata takwimu,
Tuweze kujifahamu, namna ya kujikimu,
Sensa watu na makazi, bajeti yake changia.

Kuzikusanya takwimu, kwa sensa tunafahamu,
Gharama zake ni ngumu, kote kule inadumu,
Kuchangiana muhimu, ni undugu damu damu,
Sensa watu na makazi, bajeti yake changia.

Serikali twafahamu, imeitumia zamu,
Marafiki wa muhimu, kawaita kama timu,
Sio kufanya karamu, kuhusu sense takwimu,
Sensa watu na makazi, bajeti yake changia.

Tarehe twaifahamu, Agosti ya muhimu,
Sisi sote wanadamu, humu Tanzania humu,
Kwa kutumia kalamu, zitakusanywa takwimu,
Sensa watu na makazi, bajeti yake changia.

Ishinatatu ikitimu, tarehe ile muhimu,
Tukusanyike kitimu, zipatikane takwimu,
Mipango itayoitimu, kwetu ibaki mitamu,
Sensa watu na makazi, bajeti yake changia.

Sensa ni kitu adhimu, kila taifa muhimu,
Idadi kujifahamu, maendeleo yatimu,
Tusiendelee dumu, kubahatisha takwimu,
Sensa watu na makazi, bajeti yake changia.

Nasi sote wanadamu, sensa tusijekaimu,
Tukaziacha salamu, sisi mbali tukadumu,
Tushiriki zamu zamu, kwa usahihi takwimu,
Sensa watu na makazi, bajeti yake changia.

**Na Lwaga Mwambande (KiMPAB)**
**lwagha@gmail.com 0767223602**

### MARAFIKI PANDE MBILI

Marafiki wa ukweli, ukiwaacha hulia,
Wale waso wa ukweli, hukuacha ukilia,
Hizo ndiyo pande mbili, ambazo utapitia,
Unao muda mzuri, marafiki kuwajua.

Huwezi ona dalili, kama mnashangilia,
Wakati lile na hili, vema mnajifanyia,
Kingereza Kiswahili, hapo utakisikia,
Unao muda mzuri, marafiki kuwajua.

Zionekane dalili, ya kwamba unafulia,
Au mepigwa kufuli, kipato kinatitia,
Elimu hapo mahali, mwenyewe tajipatia,
Unao muda mzuri, marafiki kuwajua.

Au uanguke chali, kwa shida kukuzidia,
Ni ukishafungwa goli, ndipo utashuhudia,
Wale marafiki kweli, na wale wa kuvizia,
Unao muda mzuri, marafiki kuwajua.

Utaicheza singeli, pekee ukigumia,
Ulodhani wa ukweli, kiona wanaishia,
Kwa matendo na kauli, mpweke utabakia,
Unao muda mzuri, marafiki kuwajua.

Uvae wako msuli, ukijisikitikia,
Au zako kanga mbili, kiuno washikilia,
Kunywa hiyo dawa kali, macho yakufungulia,
Unao muda mzuri, marafiki kuwajua.

Wametiki umefeli, jinsi ulijivunia,
Kwao ulikuwa kuli, mengi ukiwafanyia,
Uliwalisha asali, wao wakafurahia,
Unao muda mzuri, marafiki kuwajua.

Ona wanakwenda mbali, huku wewe wavilia,
Futari si pilipili, kwako waliifwatia,
Sasa umekuwa nduli, kinyama wakukimbia,
Unao muda mzuri, marafiki kuwajua.

Kama unaona mbali, mwenzako yamfikia,
Na kwako hayako mbali, usije kujilalia,
Vyako uwape kibali, baadae uje lia,
Unao muda mzuri, marafiki kuwajua.

Marafiki pande mbili, hilo lipate ingia,
Miguu ya suruali, vie waiangalia,
Inahitaji akili, yao kwako kuingia,
Unao muda mzuri, marafiki kuwajua.

**Na Lwaga Mwambande (KiMPAB)**
**lwagha@gmail.com 0767223602**





# Mkakati waja kuongeza uzalishaji mpunga

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KAMPUNI ya kuagiza na kusambaza mbolea nchini Yara Tanzania Ltd kwa kushirikiana na wadau wengine imezindua programu maalumu ijulikanayo kama AfricaConnect ambayo inalenga kuongeza tija kwa wakulima wa zao la mpunga nchini.

Aidha, kupitia programu hiyo zaidi ya wakulima 100,000 wa zao la mpunga katika mikoa yote nchini wanatarajiwa kufikiwa na huduma hiyo.

Mkurugenzi wa kampuni hiyo Winstone Odhiambo, alibainisha hayo juzi jijini Dodoma wakati wa hafla fupi ya uzinduzi wa programu hiyo ulioshuhudiwa na Naibu Waziri wa Kilimo, Antony Mavunde. Alisema moja ya malengo yao ni kubuni mbinu sahihi za kilimo ikiwamo za kidijtali zaidi na ndiyo maana wamezindua programu hiyo.

Alisema programu hiyo itawasaidia wakulima hususani wa zao la mpunga kufaidika na upatikajani fedha, pembejeo bora na uhakika wa masoko hivyo kuongeza uzalishaji nchini.

"Ndugu mgeni rasmi tunasema ni kifurushi kwa sababu Yara imeshirikiana na wadau wengine wakiwamo Equity Benki, ASA, Corteva Agriscience na Murzah Wilmar Rice Millers Ltd. Kwa kutumia application hii mkulima ataweza kupata mkopo kwa haraka, pembejeo bora, mbegu bora na viuatilifu, lakini masoko ya uhakika ili kumpa mkulima wepesi wa kufanya shughuli zake," alisema Odhiambo.

Alisema huduma hiyo pia inalenga kuhakikisha wakulima wanafuata ubora katika hatua zote za kilimo, ili wapate mazao bora kwa kutembelewa na mabwana shamba wao waliopo nchi nzima.

"Napenda kutoa rai kwa wakulima wote wa mpunga wachangamkie huduma hii kwani itakuwa na tija kubwa katika kilimo chao.

"Ni matumani yangu kuwa tutasaidiana kusambaza ujumbe huu kwa wakulima wengi zaidi ili wajiunge na mpango huu. Tayari tunaorodha ya wakulima ambao tumekuwa tukishirikiana nao lakini tungependa kuwafikia wengi zaidi," alisisitiza Odhiambo

Vilevile, alisema wanaomba wakulima wajisajili na 'application' hiyo ili kufikiwa na huduma hiyo kwa kupiga simu namba ya huduma kwa wateja 0800750188 ambayo ni bure.

Naibu Waziri wa Kilimo, Antony Mavunde, aliipongeza Yara kwa kuwa msaada mkubwa kwa serikali kwa kuisaidia kutekeleza vizuri sera ya kilimo nchini kwa kiasi kikubwa.

"Huduma hii tunayoizindua leo itaongeza uzalishaji wa mpunga kwa kiasi kikubwa na ubora utakuwa wa hali ya juu sisi kama serikali tunaunga mkono na kuwataka wakulima wote wa mpunga nchini wachangamkie fursa hii adimu,"alisema Mavunde.

Aliitaka Yara kuendelea kusajili wakulima wengi zaidi ili wafaidike na mpango huo kabambe na waangazie mazao mengine ambayo yanalimwa nchini ili kwa pamoja kuendelea kuongeza uzalishaji wa chakula kwa kufuata miongozo ya serikali.

"Napenda kuwahakikishia kuwa serikali itakuwa pamoja na nyinyi na tutawalinda dhidi ya waagizaji holela wa mbolea pembejeo nyingine zote ambao hawafuati taratibu za serikali wanataka kufaidika kwa ujanja ujanja," alisema Mavunde.

## Wito matumizi bidhaa za nchini

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

MKURUGENZI wa Huduma za Usimamizi, Bodi ya Chai Tanzania, Kemilembe Kafanabo, amewaomba Watanzania, kutumia bidhaa zinazozalishwa nchini ikiwamo zao la chai.

Rai hiyo aliitoa wakati alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kwenye maadhimisho ya Bodi ya Chai yaliyofanyika jijini Dodoma.

Kemilembe, alisema Watanzania wakitumia chai hiyo inayozalishwa nchini itaweza kuwajengea uwezo wazalishaji wakiwamo wakulima pamoja na kuinua uchumi wao kwenye maeneo yao.

Aidha, aliwataka wazalishaji hao kuhakikisha wanazalisha chai iliyo bora na viwango ili waweze kuingia kwenye ushindani wa masoko.

Alisema kuwa Bodi ya Chai Tanzania imekuwa ikitoa elimu kwa wazalishaji na watumiaji, ili watambue ubora na umuhimu wa kunywa chai kiafya.

Alisema kuwa bodi hiyo pia imejiwekea mkakati wa miaka mitano kwa ajili ya uzalishaji kutoka tani 30 hadi 60 toka mwaka 2020 hadi 2025.

Naye msimamizi mkuu wa kiwanda kinachozalisha bidhaa za chai, Kazi Yetu Limited kilichoko Mikocheni Dar es Salaam, Modesta Kaboyoka, aliwataka Watanzania kujihadhari na matumizi ya bidhaa zinazozalishwa mitaani ambazo hazina viwango kutoka TBS, ili waweze kujilinda na afya zao.

Pia aliwataka wakulima na wazalishaji wa bidhaa za chai kutengeneza yenye viwango, ili waweze kuongeza uchumi kwa ajili ya nchi yetu.

**Aidha, aliwataka wazalishaji hao kuhakikisha wanazalisha chai iliyo bora na viwango ili waweze kuingia kwenye ushindani wa masoko.**



Katibu wa Itikadi na Uenezi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Taifa, Shaka Hamudu Shaka, akizungumza na waandishi wa habari katika ukumbi wa chama hicho jijini Dodoma jana. Alisema Kamati Kuu ya CCM Taifa iliyoketi Dodoma chini ya Mwenyekiti CCM Taifa, Rais Samia Suluhu Hassan ilitoa maadhimio ya kuweka makubaliano ya uhusiano na vyama vingine vya kisiasa nchini. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Sababu ununuzi mionzi kwenye mnyororo wa chakula yatajwa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

TUME ya Nguvu za Atomiki nchini imesema sababu kubwa ya serikali kupima mionzi katika mnyororo wa chakula ni kuhakikisha chakula kinachotumika kwa matumizi ya kawaida kinakuwa salama kwa watu na wanyama.

Aidha, sababu nyingine zinazosababisha upimaji wa mionzi ni pamoja na kuangalia usafirishaji usio rasmi wa vyanzo vya mionzi ambao unaweza kusababisha uchafuzi wa vyakula namazingira kwa ujumla.

Hayo yalibainishwa na Machibya Matulanya kutoka Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania wakati wa maonyesho ya kitaifa ya mashindano ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu (MAKISATU) yaliyofanyika jijini Dodoma.

Alisema licha ya kuwa kuna faida nyingi katika mionzi, lakini mionzi isipotumika inavyotakiwa ni hatari ikiingia katika mnyororo wa vyakula kwa sababu inatoa nishati ya atomu ambayo haiwezi kuharibiwa kwa aina yoyote ile.

Matulanya, alisema kwa mujibu wa tume hiyo, viasili vya mionzi vinaweza kuathiri afya ya binadamu na wanyama ndio maana wamekuwa wakipima katika mnyororo wa chakula ili kuhakikisha kinakuwa salama kabla hakijaliwa kwa matumizi ya kawaida.

"Tunatoa elimu ya upimaji mionzi kwa wananchi katika vyakula ili watambue umuhimu wa mionzi pamoja na athari zake kama itatumika kinyume na taratibu iliowekwa,"alisema Matulanya.

Sambamba na hilo alisema wanafanya hivyo ili kulinda soko la bidhaa zetu ambazo zinauzwa nje ya nchi hasa wakati huu wa vita ya kiuchumi.

"Upimaji unatoa uwezekano wa kufuatilia kama kuna shida yoyote ikiwamo kutekeleza takwa la kupima mionzi kisheria," alisema.

Matulanya, alisema ni muhimu kupima mionzi ili kulinda soko la bidhaa zinazozouzwa nje ya nchi kwa kuzingatia ubora na viwango vilivyowekwa kulingana na miongozo na taratibu mbalimbali za serikali.

Kadhalika alisema kila mmoja anatambua kuwa ni wajibu wa serikali kuhakikisha inalinda wananchi wake hivyo kupitia tume hiyo imechukua hatua za kupima mionzi katika mnyororo mzima wa thamani ya chakula ili wananchi wake wawe salama.

"Tunajitahidi kila mara kuwakumbusha wananchi umuhimu wa kuzingatia usafirishaji salama wa mionzi ili wasichafue mazingira katika jamii," alisema Machibya.

Hata hivyo alisema ukiacha madhara lakini mionzi inafaida kubwa katika kuleta maendeleo ya kiuchumi endapo itatumiwa vizuri katika maeneo mbalimbali ikiwamo kwenye kilimo, ufugaji na afya.





# SUA, TARI zafanya utafiti kujengea uwezo wakulima

**Na Grace Mwakalinga,** KYELA

SERIKALI kupitia Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoinne (SUA) kwa kushirikiana na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo nchini (TARI), imeanza utafiti wa kuwajengea uwezo wakulima wa mpunga mkoani Mbeya kuhusu namna ya kutumia mbolea za asili kuendesha kilimo cha zao hilo.

Utafiti huo una lengo la kuwasaidia wakulima wa mpunga kuachana na matumizi ya mbolea za viwandani na badala yake watumie za asili, samadi na mboji kwenye mashamba yao ili kuongeza uzalishaji. Akizungumza juzi alipokuwa akiwaelimisha wakulima wa mpunga wa kata tatu za Makwale, Mababu na Ndobo wilayani Kyela, Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Kilimo, (SUA), Dk. Siwel Nyamba, alisema mbinu za kilimo walizozibaini baada ya kufanyika kwa utafiti, zitawasaidia wakulima kuongeza tija ya uzalishaji wa mpunga mara dufu kuliko ilivyo sasa wanapotumia mbolea za viwandani.

Dk. Nyamba alisema kuwa mbali na kuongeza uzalishaji, wakulima hao watakuwa katika nafasi nzuri ya kulinda afya ya udongo wa mashamba yao sambamba na afya za wananchi watakaotumia mazao yao kwa chakula.

"Kilimo hiki cha kutumia mbolea za asili tumekitambua kwa jina la kilimo Ikolojia, chenyewe kina faida kubwa kwa wakulima kama vile kulinda afya ya udongo na walaji, lakini kitawasaidia kuongeza uzalishaji mara dufu ikilinganishwa na kilimo cha kutumia mbolea za viwandani," alisema Dk. Nyamba.

Alisema endapo wakulima watahamasika kwa wingi kutumia mbinu hiyo ya kilimo pia watakuwa wamejiepusha na gharama kubwa ya kununua mbolea za viwandani ambazo kwa sasa ni ghali ikilinganishwa na gharama ya mbolea za asili ambazo zinapatikana kwenye mazingira yao na nyingine wanaweza kujitengenezea wenyewe.

Kwa upande wake, Mtafiti wa Afya ya Udongo, kutoka Taasisi ya Utafiti wa Kilimo nchini (TARI) Kituo cha Uyole, William Mmari, aliwataka wakulima wanaoingia kwenye mpango huo kwa mara ya kwanza kuwa wavumilivu, akidai kuwa faida zake haziji kwa haraka.

"Faida ya matumizi ya mbolea za asili haiji mara moja, hii ni kwasababu mbolea za asili zina virutubisho vyote vinavyohitajika kwenye mmea, lakini haviko kwa wingi, kutokana na hali hiyo faida yake inapatikana taratibu ikilinganishwa na wale wanaotumia mbolea za viwandani," alisema Mmari.

Alisema kuwa kwa mwaka wa kwanza mkulima anayetumia mbolea ya asili anaweza asione mafanikio makubwa, lakini kwa kadiri miaka inavyozidi kwenda shamba lake analotumia mbolea ya asili linazidi kuimarika kirutuba na baada ya miaka miwili hadi mitatu ataanza kupata mazao mengi zaidi ya anayetumia za viwandani.

Naye Ofisa Ugani wa Kata ya Mababu, Benjamin Mwaijumba, alisema ujio wa mbinu ya kilimo Ikolojia ni fursa kubwa kwa wananchi kujikwamua kiuchumi, kwa vile kitawasaidia kuepuka gharama kubwa ya kununua mbolea za viwandani huku wakipata mazao mengi kwa kutumia mbolea za asili.

"Kwa sasa mbolea za viwandani zimepanda bei mara dufu, hata mkulima akizinunua akazitumia, licha ya kupata mazao mengi, lakini hana faida yoyote kutokana na gharama za pembejeo, lakini tukilima kilimo Ikolojia kwa kutumia mbolea zetu za asili tutapata mazao mengi kwa gharama nafuu, hii ni fursa kubwa kwa wakulima kujikwamua kiuchumi," alisema Mwaijumba.

Baada ya kujengewa uwezo wa kilimo ikolojia, baadhi ya wakulima wa mpunga wilayani Kyela akiwamo, Tumain Masinga, waliishukuru serikali kwa mradi huo, kuwa utawasaidia kujilinda kiafya kwa kuepuka maradhi yanayosababishwa na kula vyakula vyenye kemikali inayotokana na matumizi ya mbolea. Hata hivyo, wakulima hao waliiomba serikali kuwasaidia kupima afya ya udongo wa mashamba yao ili waelewe aina ya mazao wanayopaswa kulima na jitihada za kiasi gani waitumie kuweka mbolea ya asili ili wapate mazao ya kuridhisha.

Aidha, walilishukuru Jukwaa la Wadau wa Kilimo wasio wa kiserikali (ANSAF), kuwaunganisha wadau mbalimbali wanaohusika katika mnyororo wa thamani wa mazao hayo kuwawezesha kuwajengea uwezo ili waendelee kuzalisha kwa tija ili kujikwamua kiuchumi kupitia kilimo cha mpunga.



Daktari wa Idara ya Mimea, Vipando na Mazao ya Bustani wa Chuo cha Kilimo Sokoine (SUA), Newton Kilasi, akiwaeleza wakulima wa mpunga katika kata za Makwale na Mababu namna kilimo cha ikolojia, kinavyozingatia matumizi ya mbolea ya asili ili kuleta tija kwa mavuno mengi, walipotembea moja ya mashamba darasa Makwale wilayani Kyela mwishoni mwa wiki. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Serikali yazindua mradi kupima afya ya udongo

**Na Grace Mwakalinga,** RUVUMA

SERIKALI kupitia Taasisi ya Utafiti wa Kilimo nchini (TARI), ikishirikiana na kampuni ya mbolea ya OCP imezindua mradi wa kupima afya ya udongo katika mikoa sita nchini wenye lengo la kuwawezesha wakulima kujua aina ya mazao wanayopaswa kulima kwenye maeneo yao na mbolea watakayotumia ili kuongeza tija katika kilimo.

Wakizungumza juzi kabla ya kuzinduliwa kwa mradi huo, wataalamu kutoka Taasisi ya Utafiti wa Kilimo nchini TARI, walieleza kuwa maeneo yatakayonufaika na mradi huo ni kupima udongo kwenye mashamba ya wakulima na kutoa ushauri wa kitaalamu namna bora ya kuzalisha mazao yao.

Mkurugenzi wa TARI Kituo cha Uyole, Dk. Tulole Bucheyeki, alisema watapima udongo na kujua vitu vilivyopo ikiwamo rutuba na athari zitokanazo na matumizi ya pembejeo na kisha kutoa ushauri kwa wakulima ili wazalishe kwa tija.

"Mradi huu wa kupima afya ya udongo utahusisha mikoa sita ikiwamo Ruvuma, Katavi, Kigoma, Arusha, Manyara na Kilimanjaro kila mkoa utafanyiwa utafiti na majibu kutolewa na kupitia utafiti huo tutatoa ushauri wa kitaalamu namna ya kukabiliana na athari zilizopatikana kwenye udongo," alisema Dk. Bucheyeki.

"Katika mradi huo jumla ya vijiji 600 katika mikoa hiyo sita itafikiwa na huduma ya upimaji wa afya ya udongo kwa wakulima 6,000," aliongeza Dk. Bucheyeki.

Mtafiti wa Kituo cha TARI kutoka makao makuu Dodoma, Magreth Mchomvi, alisema utafiti huo utasaidia kila mkulima kufahamu afya ya udongo na itamsaidia kupunguza gharama za ununuzi wa mbolea ambazo hazihitajiki katika ardhi yake.

Mchomvi alisema matokeo hayo ya utafiti, yatamsaidia mkulima kutumia eneo dogo la ardhi yake ambalo limekwisha fanyiwa utafiti kulima kwa ajili ya kuzalisha mazao mengi kwa ajili ya kukidhi mahitaji yake. Akizindua mradi huo, Mkuu wa Ruvuma, Brigedia Generali Wilbert Ibuge, alisema mpango huo wa tathmini ya utafiti wa udongo kwa Mkoa wa Ruvuma, utasaidia kuongeza uzalishaji wa mazao mbalimbali yakiwamo ya chakula na biashara na kuufanya mkoa huo kuwa kinara wa uzalishaji wa mazao nchini.

Mkurugenzi wa Kampuni ya OCP Tanzania, Dk. Mshindo Msolla, alieleza malengo ya mradi ni kutibu afya ya udongo ambayo kwa kiasi kikubwa nchini imeathirika na matumizi ya pembejeo zenye kemikali ambazo zimeathiri ardhi nyingi za kilimo.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga, Hamis Haule, alisema ni fursa kwao kwa kuwa watapata majibu ya afya ya udongo na kushauriwa ni kwa namna gani wataweza kuzalisha kwa tija na kujikwamua na umaskini kupitia shughuli za kilimo.

## Kata yakosa huduma ya mahakama wananchi watembea mbali kuifuata

**Na Grace Mwakalinga,** CHUNYA

WANANCHI wa Kata ya Sangambi, wilayani Chunya mkoani Mbeya, wanalazimika kutumia umbali wa kilomita 27, kwenda kufuata huduma ya mahakama mjini Chunya na kutokana na ukata wa fedha, miundombinu ya barabara na umbali hushindwa kufika.

Kata ya Sangambi haina huduma za mahakama ya mwanzo, wala kituo cha polisi hali inayochochea vitendo vya ukatili wa kijinsia hususani kwa wanawake na watoto.

Miongoni mwa wakazi wa eneo hilo, Glory Mwashinga, alisema kukosekana kwa huduma za vyombo vya kisheria na haki katika eneo hilo kumechangia ongezeko la vitendo vya ukatili hususani wa kingono kwa wachimbaji wa wamiliki wa migodi kuwarubuni na kuwalaghai mabinti kwa vipande vya fedha na kisha kuwaambukiza maradhi kama ugonjwa wa Ukimwi.

Mwashinga alisema kungekuwapo na mahakama watetezi wa haki za binadamu wangesimama kidedea kupinga wimbi la wanaume wenye umri mkubwa kujihusisha kimapenzi kwa mabinti wadogo na kisha kuwaharibia ndoto zao.

"Miongoni mwa vikwazo tunavyokabiliana sisi wakazi wa huku Sangambi ni kukosekana kwa huduma za mahakama na kituo cha polisi hali inayohatarisha kukosekana kwa utoaji haki kwa sababu hakuna chombo kinachosimamia au kutoa maamuzi ya haki na kuchochea vitendo vya ukatili wa kijinsia," alisema Mwashinga.

Adamson Mwampamba alisema kukosekana kwa huduma za mahakama kunachangia baadhi ya kesi kushindwa kutolewa maamuzi na wakati mwingine kuahirishwa kwa sababu ya watu kuhofia gharama za kuendesha kesi na ukizingatia umbali uliopo.

Kutokana na hali hiyo wananchi hao waliiomba serikali kuwajengea mahakama pamoja na kituo cha polisi ili kukabiliana na vitendo mbalimbali vya kihalifu kama vile, wizi na ubakaji.

Alisema kuwapo kwa vyombo hivyo vya sheria kutasaidia kudhibiti na kupunguza vya ukatili ambavyo vimekuwa vikilalamikiwa mara kwa mara licha ya kuwapo ofisi za wenyeviti wa serikali za mitaa, vijiji na kata.

Akizungumzia hali hiyo, Ofisa Mtendaji wa Sangambi, Ntundu Chapa, alikiri eneo hilo kutokuwa na huduma za kimahakama na tayari wametenga eneo lenye ukubwa wa ekari mbili kujenga mahakama.

Alisema kinachosubiriwa kwa sasa ni kufanya tathmini na gharama za ujenzi kutoka kwa viongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Chunya pamoja na wadau wengine ili kusaidia wakazi wa eneo hilo kupata haki kwa wakati.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Chunya, Tamimu Kambona, alisema kwenye bajeti ya mwaka 2022/2023 hawajatenga bajeti ya ujenzi wa mahakama ya mwanzo kwenye eneo la Sangambi na kwamba suala hilo atalichukua na kwenda kuwashirikisha watumishi wa mahakama wa wilaya hiyo kujua namna ya kufanya ili kuwasaidia wakazi hao.

Uwepo wa mahakama ya mwanzo pamoja na kituo cha polisi katika Kata ya Sangambi kutasaidia kudhibiti vitendo mbalimbali vya uhalifu na ukatili wa kijinsia kwa sababu eneo hilo shughuli zake kubwa ni za uchimbaji wa madini ya dhahabu.





# 'Kukuza usawa kijinsia kunahitaji nguvu ya ziada'

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Riziki Pembe Juma, amesema kuwa nguvu za ziada zinahitajika ili kufikia malengo ya kimataifa na kitaifa katika kukuza usawa wa kijinsia na uwezeshaji wa wanawake nchini. Aliyasema hayo wakati akifungua mafunzo ya uongozi wa kimabadiliko kwa makatibu wakuu na manaibu makatibu wakuu wa Serikali ya Zanzibar yaliyofanyika Mkoa wa Kaskazini, Unguja.

Alisema uwapo wa utashi wa kisiasa kupitia viongozi wakuu wa nchi umechochea mafanikio katika kuleta usawa wa kijinsia na uwezeshaji kwa wanawake.

Alisema Zanzibar imekuwa na sera inayotoa miongozo ya uzingatiaji wa masuala ya jinsia na uwezeshaji wa wanawake tangu mwaka 2001 na hivi sasa kuna sera ya jinsia ya mwaka 2016 ambayo serikali ina mpango wa kuzifanyia mapitio ili iende sambamba na mabadiliko ya sera na sheria zingine.

Akiyataja mafanikio mengine alisema ni kufanyika kwa mabadiliko ya sheria hasa zinazohusu masuala ya kupambana na vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia zikiwamo Sheria ya Jinai namba 6 ya mwaka 2018, Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai namba 7 ya mwaka 2018 na Sheria ya Mahakama ya Kadhi namba 9 ya mwaka 2017 ili kuimarisha upatikanaji wa haki kwa waathirika wa vitendo hivyo.

Alisema Zanzibar ikiwa ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeridhia mikataba na maazimio mbalimbali ya kitaifa na kikanda inayolenga katika kufikia usawa wa kijinsia na uwezeshaji wa wanawake katika ngazi zote.

Waziri Pembe alisema ni matarajio yake kwamba washiriki wa mkutano huo wataboresha mazingira katika tasisi zao yatakayowezesha matokeo ya usawa wa kijinsia ndani ya sekta hizo pamoja na kuimarisha ushirikiano utakaofanya matokeo endelevu.

"Nyinyi ndiyo watendaji wakuu katika wizara na ipo changamoto ya ubaguzi hivyo ni matarajio yangu kuwa mtakuwa mnasimamia masuala ya kijinsia kwa nguvu zote," alisema.

Naye Naibu Mwakilishi Mkaazi wa UN Women nchini Tanzania, Julia Broussard, alisema Tanzania Bara na Zanzibar imepiga hatua kubwa katika kuimarisha usawa wa kijinsia na kuimarisha uongozi kwa wanawake.

Alisema UN Women itaendelea kushirikiana na serikali zote mbili katika jitihada za kuishajihisha usawa wa kijinsia na kuwawezesha wanawake kufikia maendeleo yanayohitajika hasa katika kupambana na umaskini.

Alisema ni matumaini yake kwamba mkutano huo utakuja na mikakati imara ya kufikia usawa wa kijinsia na kutatua changamoto zinazojitokeza kwa upande wa wanawake na watoto ikiwamo udhalilishaji na kuongeza idadi ya wanawake katika vyombo vya uamuzi.



Spika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Zubeir Ali Maulid, akizungumza na Balozi Mdogo wa China nchini Tanzania, Zhang Zhisheng, alipotembelewa na balozi huyo ofisini kwake Chukwani kwa ajili ya kujitambulisha pamoja na kuendelea kuimarisha ushirikiano uliopo baina ya China na Zanzibar. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Maboresho makubwa uongozi yaja ZECO

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Maji, Nishati na Madini, imesema Shirika la Umeme lipo katika maboresho makubwa ya uongozi ikiwa na lengo la kufikisha huduma zake vijijini na visiwa vidogo Unguja na Pemba.

Hayo yalisemwa na Naibu Waziri wa wizara hiyo, Shaaban Othman, katika kikao cha Baraza la Wawakilishi, wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Jimbo la Kojani, Hassan Hamadi, aliyetaka kujua lini Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO), litafikisha huduma zake katika visiwa vidogo kwa ajili ya kuleta mabadiliko makubwa ya maendeleo na kiuchumi ikiwamo uchumi wa buluu.

Othman alisema ZECO imejipanga kuhakikisha huduma muhimu za usambazaji wa umeme zinafikishwa hadi vijijini na wizara imetenga fedha za usambazaji wa nishati hiyo kupitia fedha za ahuweni kupambana na ugonjwa wa COVID -19.

Alisema hadi sasa visiwa viwili vya Unguja vimepata huduma za usambazaji wa umeme vijijini vikiwamo kisiwa cha Tumbatu na Uzi hatua ambayo imesaidia kuleta mabadiliko makubwa ya maisha ya wananchi na sekta ya uvuvi.

Alisema juhudi zinaendelea kwa upande wa Pemba kuona huduma ya umeme inafikishwa vijijini ili kuleta mageuzi ya wananchi kwa maendeleo ya taifa.

Alisema tayari serikali imefanikiwa kufikisha huduma za umeme katika kisiwa cha Kojani ambacho ni wilaya ndogo katika Mkoa wa Kaskazini Pemba.

**Alisema juhudi zinaendelea kwa upande wa Pemba kuona huduma ya umeme inafikishwa vijijini ili kuleta mageuzi ya wananchi kwa maendeleo ya taifa.**

# Mabaraza ya vijana yatahadharishwa kutumika kisiasa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imesema Mabaraza ya Vijana yapo kitaifa na hayakuundwa kwa misingi ya kisiasa na wizara ipo katika hatua za mwisho za kufanya marekebisho ya sera kwa ajili ya kuleta ufanisi na maendeleo ya kiuchumi.

Hayo yalisemwa na Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, Tabia Maulid Mwita, wakati akijibu hoja za wajumbe wa Baraza la Wawakilishi waliochangia makadirio, mapato na matumizi ya bajeti ya wizara kwa mwaka wa fedha 2022-2023 katika kikao cha baraza hilo.

Alisema serikali imeunda mabaraza ya vijana kwa ajili ya kuleta mabadiliko makubwa ya kiuchumi na kuona vijana wanapiga hatua kubwa ya maendeleo katika utekelezaji wa miradi yao.

Alisema mabaraza ya vijana muundo wake upo chini ya Idara ya Maendeleo vijana chini ya wizara na hayana uhusiano wowote na masuala ya chama katika uendeshaji wake.

"Mheshimiwa Spika napenda kumjibu Mwakilishi wa Jimbo la Pandamni, Professa Omar Fakih Hamad, kwamba mabaraza ya vijana yapo katika kiwango cha kitaifa na sio kisiasa...mimi ndiye ninayesimamia muundo wake yanajumuisha vijana wote wasiokuwa na mwelekeo wa kiitikadi wa vyama," alisema.

Alisema Mabaraza ya Vijana yanatarajiwa kupata fedha za UVIKO-19 ambazo zitatumika katika kuibuwa miradi mbalimbali ya kiuchumi katika sekta mbalimbali ikiwamo kilimo na uvuvi.

Akichangia kuhusu Mabaraza ya Vijana, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Uwezeshaji Kiuchumi na Uwekezaji, Mudrik Ramadhan Soraga, alisema serikali tayari imeunda wakala wa uwezeshaji wananchi kiuchumi ambao miongoni mwa kazi zake ni kutoa mikopo kwa vikundi mbalimbali kuona vinapiga hatua kubwa ya maendeleo ya kiuchumi.

Soraga alisema tayari wakala wa uwezeshaji wananchi kiuchumi umeanza utekelezaji wa majukumu yake na upo katika mchakato wa kuyafikia makundi yote ikiwamo Mabaraza ya Vijana yaliyopo Unguja na Pemba.

Alizitaja kazi za wakala wa uwezeshaji wananchi kiuchumi ni pamoja na kutoa elimu kwa vikundi na wajasiriamali pamoja na kuibua mchanganuo wa miradi pamoja na kutafuta masoko.

"Mheshimiwa Spika nataka niwaambie wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwamba muswada wa kuanzishwa kwa wakala wa uwezeshaji wananchi kiuchumi umeanza kazi baada ya kutiwa saini na Rais na kwa sasa tupo katika mchanganuo wa miradi ya vikundi vya wajasiriamali ambapo mabaraza ya vijana yamo," alisema.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA RESULT SLIP



**LUCY DANSTAN MAKANGE** anatangaza kupotea kwa RESULT SLIP yenye index namba **S.5462/0026** iliyotolewa na Baraza la Mitihani La Taifa kupitia ST. WILBALDA SECONDARY SCHOOL mwaka 2021. Yeyote atakeiona atoe taarifa kituo cha polisi. POLISI TAARIFA: **DAR/MBA/RB/192999/2022**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ADAM RAMADHANI NDAKI** anatangaza kupotea kwa kadi yake ya gari yenye namba za usajili **T 993 DNL – TOYOTA ALPHARD.** Chassis namba **ANH150011922.** Engine namba **2AZ1167710.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya Polisi: **MWA/NY/RB/164056/2022.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO MJINI**
**ILIYOPO MOROGORO**
**TANGAZO LA KUITWA SHAURINI**
**SHAURI LA MADAI NAMBA 346......................2020**
**MDAI NZIMJAGWA J MKODO**
**DHIDI YA**
**MDAIWA CHARLES JOHN**
**KWA CHARLES JOHN**

### OMBI LA MDAI CHARLES JOHN

Unatakiwa kuhudhuria hapa Mhakamani katika shauri tajwa hapo juu bila kukosa. Shauri limepangwa kusikilizwa mnamo **tarehe 24 Mwezi 05 Mwaka 2022 Saa 8:30 Asubuhi**

Angalia kama*hukuhudhuria/hamkuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu, Mahakama ikathibitisha kama umepokea /mmepokea kuitwa shaurini, hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa/mmeshindwa

Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe **19 Mwezi 4 Mwaka 2022**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**WILLIAM MICHAEL MATHAYO**

Anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye namba za usajili **MC.762 CXR.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo jirani yake. Taarifa ya jeshi la polisi. **KAH/RB/ TRA/269/022.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**ISLAM ATHUMANI RAMADHANI** anatangaza kupotea kwa cheti cha chuo CERTIFICATE chenye usajili namba **NS3843/0043/2011** kilichotolewa na NACTE kupitia CLINICAL OFFICERS TRAINING CENTRE MTWARA mwaka 2019. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **DAR/CHA/ R B/194547/2022**

**UYOLE HOSPITAL LIMITED**
**NAMBA YA KAMPUNI: 28839**
**TANGAZO LA KUFUNGA KAMPUNI**

Bodi ya wanahisa wa **UYOLE HOSPITAL LIMITED** imeamua kufunga shughuli zake za biashara rasmi kuanzia tarehe **20/05/2022.** Kwa tangazo hiliwatu wote ambao wanaidai Uyole hospital limited wapeleke madai yao ndani ya siku 90 kuanzia tarehe ya tangazo hili katika ofisi za kampuni zilizopo Uyole, Mbeya.

Aidha wawasiliane na mfilisi wa kampuni kwa kupitia mawasiliano:

**JINA : VICTOR CHERUBIN MMOLE MKUMBE**
**NAMBA YA SIMU: 0784863538**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**SHUNI MBARAKA SALEH** anatangaza kupotea kwa Kadi yake ya gari aina ya Toyota Kluger yenye no za usajili T556 DWS chassis no ACU200014137 kwa yeyote atakaeiona au kuokota atoe taarifa Kituo chochote Cha polisi . Taarifa ya Polisi **POLISI TAARIFA: DSM /PHQ/RB/190449/2022**

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**KANDA YA DODOMA**
**SHAURI LA RUFAA YA ARDHI NA.80/2019**
**SAIMON N. CHIHOMA...................... MRUFANI**
**DHIDI YA**
**ABEL DEULE...........................MJIBU RUFAA**
**KWA: ABEL DEULE**
**POPOTE PALE ALIPO**
**YAH: TAARIFA YA KUTAJWA KWA SHAURI LA RUFAA NA.80/2019 MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**

**UNAFAHAMISHWA KWAMBA:** Shauri tajwa hapo juu litatajwa Mahakama Kuu Tanzania, Kanda ya Dodoma, mbele ya **Mh.Jaji A.S.KAGOMBA**, wa Mahakama Kuu ya Tanzania Dodoma,saa tatu (3.00) kamili asubuhi siku ya Jumatatu tarehe 7/06/2022.
**HIVYO BASI:** Unatakiwa ufike mwenyewe au Wakili wako siku hiyo iliyotajwa bila kukosa.
**NA ENDAPO**: hautafika mwenyewe au wakili wako siku hiyo iliyotajwa inatosha kumaanisha kwamba shauri hili litashughulikiwa na Mahakama kama itakavyoamua pasipo wewe au Wakili wako kuwepo.
**IMETOLEWA:** Kwa mkono wangu na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 21Mwezi wa **APRIL,2022**

**NAIBU MSAJILI**
**KANDA YA DODOMA**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA MWANZO IRINGA MJINI**
**SHAURI LA TALAKA NA 12/2022**

**NAY EMMANUEL SINDILA...............MDAI**
**VS**
**FREDRICK MNGUJI.................MDAIWA**

**MAOMBI YA TALAKA**

Unatakiwa kufika mahakamani tarehe 26/05/2022 saa 2:30 asubuhi kwa ajili ya shauri la talaka usipofika, shauri litadikilizwa upande mmoja na kutolewa maamuzi.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 13/05/2022.

.............................................................
**HAKIMU MAHAKAMA YA MWANZO IRINGA MJINI.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya Bukoba kituo cha Bukoba Mjini**

**Shauri la Madai Na. 21 la 2022**

**Jina la mdai ....................................Willimina Calist**

**Jina la Mdaiwa .......................... Adronick P. Kahigi**

**KUITWA SHAURINI KWA MDENI MHUKUMIWA**

Kwa Adronick P. Kahigi, kwamba mdai ameleta maombi mbele ya Mahakama hii kwa ajili ya utekelezaji wa hukumu ya shauri tajwa hapo juu. Unatakiwa kufika mbele ya Mahakama hii tarehe 03 Mwezi 06 mwaka 2022 kueleza kwa nini hukumu isitekelezwe dhidi yako.

Hati hii imetolewa kwa amri na muhuri wa Mahakama leo tarehe 23 mwezi 05 mwaka 2022.

..................................
**HAKIMU**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**katika Mahakama ya Mwanzo ya wilaya ya DODOMA**
**kituo cha DODOMA MJINI, Mkoa DODOMA**
**Shauri la Madai Na.50/2022**
**Jina la mdai DINAH ABDALLAH NJOVU**
**Jina la Mdaiwa DOTTO HAMIS SHOMARI**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu Madai katika Mahakama za Mwanzo)**

**Kwa. DOTO HAMIS SHOMARI**
**MAGOMENI – DAR - ES –SALAAM.**

**Kwa kuwa Mdai ameleta madai yake kwamba**
**MADAI YA TALAKA MGAWANYO WA MALI MATUNZO**

Kwa hiyo unahitajika kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii siku ya tarehe 06/06/2022 saa 2:30 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/ mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
**ANGALIZO:** kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na itadhibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa amri yangu na Muhuri wa Mahakama hii leo 23/05/2022.


**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676**

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharasma yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# Uganda haitadhibiti gharama za maisha

**KAMPALA,** UGANDA

RAIS wa Uganda, Yoweri Museveni, amesema serikali haitaingilia kati hali ya sasa ya kiuchumi na kupanda kwa gharama ya maisha nchini humo.

Bei za bidhaa za mafuta, mali ghafi inayoagizwa kutoka nje ya nchi, pamoja na chakula, zimekuwa zikipanda katika miezi michache iliyopita.

Mfumko wa bei nchini Uganda umefikia asilimia 4.9, kiwango hiki cha juu zaidi kuwahi kushuhudiwa tangu mwaka 2017.

Katika hotuba yake kwa taifa kupitia televisheni juzi usiku, Museveni alisema ruzuku ya serikali au kuondolewa kwa ushuru wa bidhaa zinazoagizwa nje ya nchi kutaporomosha uchumi.



Kutumia kwa akiba ya kitaifa kwa ununuzi wa bidhaa hizo za bei ghali kutakuwa na athari kubwa, kiongozi huyo alieleza.

Akiba ya sarafu ya kigeni nchini Uganda kwa sasa ni zaidi ya bilioni nne. Museveni (pichani) alisema nchi inatakiwa kutumia bidhaa za kuagizwa ambazo inaweza kumudu pekee.

Pia aliwashauri wananchi kubadilisha ngano ya bei ghali badala ya vyakula vinavyopatikana nchini kama vile mtama, mahindi, ndizi mbichi na mihogo.

Sehemu kubwa ya Uganda ina uwezo wa kuzalisha vyakula kwa wingi, familia nyingi zinategemea kilimo cha kujikimu.

Kati ya mwaka 2020 na 2021, kilimo kilichangia takribani asilimia 23.7 ya Pato la Taifa la nchi. Lakini hata bei za vyakula vinavyozalishwa nchini vimekuwa vikipanda, hasa mijini, kutokana na gharama za usafirishaji.

Raia wa Uganda wanalazimika kununua kiasi kidogo cha vitu vya msingi au kuegesha magari yao ili kukabiliana na mzozo huo.

# Russia yadaiwa kukodi wataalamu wa mabomu

**LONDON,** UINGEREZA

ZAIDI ya wataalamu 50 kutoka Syria wenye uzoefu katika utengenezaji na utumiaji wa mabomu ya mapipa wamewasili na kufanya kazi nchini Russia kwa wiki kadhaa.

Kulingana na taarifa zilizotolewa na gazeti la Guardian la Uingereza, likiwanukuu maofisa wa Ulaya wakisema wataalamu hao wanashirikiana na jeshi la nchi hiyo.

Taarifa hiyo ilieleza wataalamu wa utengenezaji wa silaha hiyo ya kiholela, ambayo iliharibu sehemu kubwa ya Syria wakati wa vita vya wenyewe kwa wenyewe, walitumwa nchini humo kusaidia kuendeleza operesheni za kivita nchini Ukraine.

Uwepo wao nchini Russia kunaweza kuwa moja ya sababu zinazoelezea za Marekani na Ulaya kwamba jeshi la Russia linaweza kujiandaa kutumia silaha za kemikali nchini Ukraine.

Kulingana na wataalamu hao, kutokana na kiwango cha chini cha usahihi, mabomu ya pipa hutumiwa hasa katika hali ya rasilimali ndogo na ukosefu wa silaha nyingine. Silaha ya aina hiyo ilitumika na kuleta madhara makubwa nchini Syria.

"Tunajua kwamba kuna uwezekano wa kutumia mabomu ya pipa, lakini ikiwa jeshi la Russia litatumia huko Ukraine, watapoteza kwa sababu tutajua ni nani aliyefanya hivyo, na uwezekano mkubwa bado watauawa," maofisa wa Ulaya ambao hawakutajwa waliiambia The Guardian.

### Mwenyekiti AU kuzuru Russia, Ukraine

RAIS wa Senegal Macky Sall, amesema atasafiri katika nchi za Russia na Ukraine hivi karibuni kama mwenyekiti wa Umoja wa Afrika.

Sall alisema kuwa amepokea mamlaka ya wakuu wengine wa nchi wa AU kufanya safari hizo.

Katika mkutano wa pamoja na Kansela wa Ujerumani anayezulu Afrika Olaf Sholz, alisema Afrika ina nia ya kuona amani kupitia mazungumzo kati ya Ukraine na Russia.

Kiongozi huyo wa Senegal alisema Russia ilitoa mwaliko wa kufanya ziara huku rais wa Ukraine akieleza haja ya kuwasiliana na wakuu wa nchi za Afrika.

Mgogoro wa Russia na Ukraine umekatiza usambazaji wa nafaka na mafuta ya kupikia, na hivyo kuzidisha uhaba wa chakula hasa katika nchi maskini za Afrika kutokana na kupanda kwa bei.

Bei ya mafuta duniani pia imepanda kutokana na hilo, na kuongeza mzigo wa gharama kwa nchi nyingi.

### Ukraine inaweza kupoteza wanajeshi 100 kila siku

Ukraine huenda inapoteza kati ya wanajeshi 50 hadi 100 katika eneo la mashariki kila siku.

Rais Volodymyr Zelensky, alisema hayo wakati wa mkutano na waandishi wa habari Juzi.

Alisema waliouawa walikuwa wakilinda Ukraine katika mwelekeo mgumu.

Zelensky hakufafanua zaidi lakini maoni hayo yanaonekana kuwa ni dalili ya uwepo wa hasara za kijeshi na kuonekana eneo hilo kuna mapigano makali.

Vikosi vya Russia vimeongeza juhudi zao za kuteka miji ya eneo la Donbas mashariki, kwa kuulenga mji wa Severodonetsk.

### Hakuna wa kunitenganisha na mume wangu, Mke wa Zelensky

Mke wa Rais wa Ukraine, Olena Zelensky amefanya mahojiano ya nadra akiwa na mumewe Volodymyr Zelensky.

Hii ni mara ya pili kwa wanandoa hao kuonekana wakiwa pamoja tangu kuanza kwa vita nchini Ukraine.

Familia ya Zelensky ilipelekwa mahali pasipojulikana kwa sababu za kiusalama.

Olena alieleza katika video kuwa, chochote hakiwezi kumchukua mumewe hata vita pia haviwezi. Aliongeza kama familia nyingine nchini Ukraine, wameathirika pia na vita hivyo.

Lakini alisisitiza kuwa anaelewa umuhimu wa kazi yake.

"Hatujaonana kwa zaidi ya miezi miwili, tunazungumza tu kwa simu, na nimefurahi sana kwa nafasi hii, kwani mahojiano haya angalau yanafanya tunakuwa pamoja," alisema Olena. **BBC**



Mvua imesababisha mafuriko na kuharibu miundombinu katika mji wa Natal nchini Afrika Kusini juzi. **PICHA: BBC**



Wanafamilia ya kanali Sayad Khodai wakiwa wamezunguka gari lake baada ya kuuawa akiwa ndani ya gari hilo. **PICHA: BBC**

# Kanali wa jeshi Iran auawa

**TEHRAN,** IRAN

KANALI wa Jeshi la Walinzi wa Mapinduzi ya Iran (IRGC), Sayad Khodai, ameuawa kwa kupigwa risasi mjini Tehran.

Watu wawili wenye silaha waliokuwa kwenye pikipiki wanaripotiwa kumpiga risasi Kanali Khodai mara tano kwenye gari nje ya nyumba yake.

Hakuna kundi lililodai kuhusika na shambulizi hilo la juzi, huku msako unaendelea kuwatafuta watu hao wenye silaha.

Kumekuwa na ukiukaji wa usalama nchini humo tangu 2020 wakati mwanasayansi mashuhuri wa nyuklia alipouawa.

Picha kutoka eneo la tukio zinaonyesha mwanaume aliyemwagika damu akiwa amejilaza kwenye gari huku akiwa amejifunga mkanda wa kiti.

Kanali Khodai alikuwa mwanachama mkuu wa Kikosi cha wasomi cha Quds, tawi la IRGC ambao kinaendesha operesheni nje ya nchi.

Marekani inakishutumu kikosi hicho kwa kuunga mkono mashirika ya kigaidi na kuhusika na mashambulizi katika eneo la Mashariki ya Kati. **BBC**

# MPOLE AMSHANGAA MAYELE KULALAMA MABEKI KUMKAMIA

**Na Adam Fungawango**

KINARA wa mabao kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, George Mpole, amepingana na kauli ya straika wa Yanga, Fiston Mayele kuwa mabeki wanakamia sana, akidai hakuna mlinzi yeyote atakayeweza kumwachia mshambuliaji afunge kirahisi.

Akizungumzia maendeleo na mafanikio yake kwenye ligi msimu huu, wakati huu akiwa tayari mpaka juzi amepachika mabao 14 kwenye Ligi Kuu, akichaguliwa pia kuwa mchezaji bora wa mwezi uliopita, Mpole mchezaji wa zamani wa Majimaji, na Polisi Tanzania kwa sasa akiichezea Geita Gold FC, alisema mabeki wa Tanzania wana viwango vya hali ya juu, hivyo hawakamii na wala hawalegezi, ila ni kwa straika mwenyewe kuwasababisha wafanye makosa.

"Kwangu mimi siwezi kusema kama mabeki wa Ligi Kuu wanakamia au wanalegeza, naweza kusema tu wana viwango vikubwa, lakini kila mechi zinavyozidi kupungua kila timu inakuwa na presha kubwa, inahitaji kukaa sehemu nzuri, kwa hiyo hakuna beki ambaye atakubali kumpita au kufungwa kirahisi, hivyo ni lazima umlazimishe afanye makosa uweze kuyatumia wewe kama mshambuliaji.

"Mechi zimebaki chache tu ligi iishe, kwa hiyo ninavyoona umakini umeongezeka tu kwenye timu, ndiyo maana inaonekana ni kama wanakamia," alisema Mpole.

Alisema hajawahi kuona beki ambaye anajipanga kumkaba straika kwa kumkamia na mwingine amkabe kawaida.

Hivi karibuni straika wa Yanga, Mayele ambaye kabla ya mechi ya jana dhidi ya Biashara United alikuwa na mabao 13, alisema kuwa mabeki wa Ligi Kuu wamekuwa wakimkamia ndiyo maana kwa siku za karibuni ameshindwa kufunga mabao, hata hivyo alifunga Ijumaa iliyopita dhidi ya Mbeya City, baada ya mechi nne kupita.



Wanafunzi wa Shule ya Sekondari Juhudi, ya Gongo la Mboto jijini Dares Salaam, wakifanya mazoezi ya kucheza mpira wa Magongo kwenye viwanja vya Jakaya Kikwete Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Tanzania yaanza vema Baseball 5 Afrika*

**Na Shufaa Lyimo**

TIMU ya Taifa ya Tanzania ya mchezo wa Baseball, imeanza vema mashindano ya Afrika ya Baseball 5 baada ya kuifunga Zambia kwa ushindi wa pointi 18-4, mchezo ambao ulipigwa jana asubuhi kwenye Uwanja wa Ndani wa Taifa jijini Dar es Salaam.

Katika mashindano hayo yaliyoanza kutimua vumbi Dar es Salaam huku yakitarajiwa kumalizika Ijumaa wiki hii, awali Tanzania ilikuwa icheze dhidi ya Misri, lakini ratiba hiyo ilibidi ibadilishwe kutokana na Wamisri hao kuchelewa kufika.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, baada ya kumalizika kwa mchezo huo Kocha Mkuu wa timu ya Taifa ya Baseball ya Tanzania, Maclina Mutabuzi, alisema amefurahishwa na matokeo hayo kwani maandalizi ya muda mrefu waliyoyafanya yamewasaidia kupata ushindi huo.

"Nimeyapokea kwa furaha matokeo haya, tumeanza vizuri, wachezaji wangu walipambana hatimaye tukaibuka na ushindi huo kwa kuwazidi kwa pointi nyingi," alisema Mutabuzi.

Alisema licha ya wapinzani wao wa awali, Misri kushindwa kutokea, haijawagharimu kwani uongozi ulikaa haraka na kuamua kupanga ratiba nyingine.

Alisema kwa matokeo hayo mpaka sasa tayari wameona mwanga wa kufuzu kushiriki Kombe la Dunia litakalofanyika Septemba mwaka huu nchini Mexico.

Kwa upande wa nahodha wa timu hiyo, Abdul Mounim Ally, alisema wamefurahi kupata ushindi huo na kwamba lengo lao ni kusonga mbele na hatimaye kufuzu.

"Tumefurahi kushinda mchezo wetu wa kwanza japo wapinzani wetu walijipanga na sisi tulijipanga," alisema Ally.

Nahodha huyo alisema amejifunza mambo mengi kupitia mashindano hayo kutoka kwenye timu ambazo zimekuja kushiriki.

"Nimejifunza aina ya uchezaji kutoka kwa wachezaji wa mataifa mengine, vile vile nimeona wanashangilia sana mataifa yao na sisi Watanzania tunapaswa kuiga mfano huo," alisema.

Mchezo mwingine ambao ulichezwa jana ni kati ya Ghana na Tunisia, ambapo Watunisia hao waliibuka na ushindi.

Mashindano hayo ambayo ni mara ya kwanza kufanyika nchini, yataendelea tena leo.

Tanzania imepangwa Kundi B na timu ya Burkina Faso, Zambia, Kenya na Misri ambayo haijafika pointi zao zitagawanywa kwenye timu zote ambazo zilipangwa kucheza nayo.

## Juma Kaseja achambua ubora Simba, Yanga

**Na Adam Fungamwango**

GOLIKIPA wa zamani wa klabu za Simba na Yanga, Juma Kaseja ametoa tathmini yake kwa timu kongwe nchini, akidai msimu huu Yanga ina kikosi bora na wana wachezaji ambao wamekuja kuwasaidia kwenye mapungufu waliyokuwa nayo kwa muda mrefu, huku akisema kuwa wachezaji wa Simba wamechoka.

Kuhusu Yanga ambayo aliichezea msimu wa 2014/15, Kaseja alisema: "Yanga wana timu nzuri msimu huu na wana wachezaji ambao wamekuja kuwasaidia kweli. Angalia golini kuna mtu anayesaidia sana eneo hilo na ndiyo sehemu ambayo walikuwa wanahangaika kwa muda mrefu, kusema kweli golini wamepata mtu sahihi na kwa straika ambaye amekuja kutibu eneo la kufunga mabao, ukisema Yanga siyo nzuri utakuwa unataka tu kusema lakini wanacheza vizuri na wana timu nzuri."

Akiizungumzia Simba, alisema: "Simba naona wamechoka, wamecheza mfululizo sana, michuano mbalimbali ya ndani ya ya kimataifa, wana timu nzuri, lakini inatatizwa sana na uchovu wa wachezaji wake, kwa muda mrefu wamekuwa wakicheza mechi za kimataifa na za ndani bila kupumzika," alisema kipa huyo ambaye aliichezea timu hiyo kwa miaka 11 kutoka 2003 hadi 2014.

## Mabondia watatu kuzipiga Uingereza

**Na Shufaa Lyimo**

MABONDIA watatu wa Tanzania wanatarajiwa kwenda kushiriki mashindano ya Jumuiya ya Madola ya Ngumi za Ridhaa nchini Uingereza yatakayoanza kutimua vumbi Mei 27-31, mwaka huu.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Katibu Mkuu wa Shirikisho la Ngumi za Ridhaa nchini (BFT), Muhamed Abubakari, aliwataja mabondia hao kuwa ni Alex Michael ambaye atapigana katika uzani wa kilo 63.5, Kassim Selemani Bundike (kilo 71) pamoja na Yusuph Lucas Changarawe atakayepigana uzito wa kilo 80.

"Mabondia wapo sita kambini ambao wanajiandaa na mashindano ya kimataifa ya Ngumi za Ridhaa yatakayoanza kutimua vumbi Mei 27-31, mwaka huu, lakini hao niliowataja ndio ambao wamepangwa kwenda kuiwakilisha Tanzania kwenye mashindano ya Jumuiya ya Madola," alisema Abubakari.

Katibu huyo alisema malengo yao ni kuona mabondia hao warudi na medali za ushindi nyumbani kwa kufanya vizuri kwenye mashindano hayo.

Aidha, alisema anaishukuru serikali kusikia kilo chao cha muda mrefu cha kutopata medali za ushindi miaka mingi kwa kuamua kuwadhamini mabondia kuanzia kambi, malazi pamoja na chakula.

HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### RICE KUBAKI WEST HAM

DECLAN Rice, 23, atabaki West Ham licha ya Manchester United kuonyesha nia ya kutaka kumsajili nyota huyo wa England. ***(Mirror)***

### ALONSO AITAKA BARCA

MLINZI wa Chelsea, Marcos Alonso, 31, anataka kuhama Stamford Bridge baada ya kuwa huko kwa miaka sita, na Barcelona wamepiga hatua katika mazungumzo kuhusu makubaliano binafsi. ***(Fabrizio Romano, Twitter)***

### TCHOUAMENI ANUKIA LIVER

KIUNGO wa kati wa Monaco na Ufaransa, Aurelien Tchouameni, 22, ameafikiana na Liverpool, lakini klabu hiyo bado inakabiliwa na kibarua kigumu kumpata mchezaji huyo ambaye pia anawaniwa na Real Madrid. ***(Mirror)***

### PHILLIPS ATAKIWA VILLA

ASTON Villa wamemweka kiungo wa kati wa Leeds United, Kalvin Phillips, 26, katika orodha ya wachezaji inaowalenga. ***(Telegraph)***

### LEAO AWANIWA MADRID

REAL Madrid wanataka kumsajili mshambuliaji wa AC Milan, Rafael Leao, 22, baada ya Kylian Mbappe kuamua kubaki Paris St-Germain. ***(Marca)***

### LINGARD NA WEST HAM

WEST Ham wamewasilisha dau la kutaka kumnunua winga wa Manchester United, Jesse Lingard, 29, ambaye mkataba wake unamalizika Juni. Lingard alifunga mabao katika mechi 16 za Ligi Kuu wakati alipokuwa na 'Wagonga Nyundo' hao wa London msimu wa 2020-21. ***(Mail)***

### LENO AWANIWA BENFICA

BENFICA wanataka kumsajili kipa wa Arsenal, Bernd Leno, 30, ambaye ameshika nafasi ya pili nyuma ya Aaron Ramsdale kama chaguo la kwanza la kocha Mikel Arteta. ***(Correio da Manha)***

### TELLES KURUDI PORTO

FC Porto wanapania kumsajili tena kiungo wa Manchester United na Brazil, Alex Telles, 29, msimu huu wa majira ya joto. ***(Correio da Manha)***

### SALIBA KUBAKI ARSENAL

MLINZI wa Arsenal, William Saliba, 21, anataka kubaki Marseille, ambako amekuwa akicheza kwa mkopo. ***(Goal)***

### EKITIKE NA NEWCASTLE

KLABU ya Newcastle imejizatiti kumsajili mshambuliaji, Hugo Ekitike, 19, ambaye anacheza kule Reims - lakini wanakabiliwa na upinzani kutoka kwa Borussia Dortmund. ***(Fabrizio Romano, Twitter)***

### KAMARA SAFI VILLA

KLABU ya Aston Villa wanakaribia kumsajili kiungo wa kati, Boubacar Kamara, 22, kutoka Marseille kwa uhamisho wa bure. ***(Matteo Moretto, Twitter)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# IBRAHIMOVIC: NITAENDELEA KUCHEZA MSIMU MWINGINE

**●●● Autoa ubingwa wa Milan Serie A kwa aliyekuwa wakala wake Mino Raiola, asema...**

**MILAN,** Italia

ZLATAN Ibrahimovic amebainisha kuwa mpango wake ndani ya AC Milan umekamilika wakati 'Rossoneri' hao wakitawazwa kuwa mabingwa wapya wa Serie A kwa mara ya kwanza baada ya miaka 11 - lakini mkongwe huyo hajakataa uwezekano wa kuendelea kucheza msimu mwingine.

**Mshambuliaji huyo wa Sweden mwenye umri wa miaka 40, alianza kipindi cha pili cha maisha yake ya soka akiwa na Milan Desemba 2019, na amesema hiyo ilikuwa kwa amri ya wakala wake wa muda mrefu, Mino Raiola, ambaye alifariki mwishoni mwa Aprili.**

Ibrahimovic alilitoa taji hilo la Milan kwa Raiola, ambaye alisema alimuunga mkono kwenda kuisaidia timu hiyo. Mchezaji huyo wa zamani wa Juventus na Inter Milan pale San Siro amekuwa na matokeo ya ajabu, akiwa na wingi wa mabao mapema na kuinua ari kwenye klabu hiyo na kuweka mwelekeo wa mafanikio yaliyofuata.

Msimu uliopita, Ibrahimovic alifunga mabao 16 katika mechi 26 huku Milan ikimaliza nafasi ya pili kwenye Serie A, na msimu huu pia akiwa amecheza mechi 26, akianza 12 pekee na kutikisa nyavu mara nane. Msimu huu alikuwa akisumbuliwa na majeraha ya mara kwa mara, lakini ufanisi wa Ibrahimovic ulikuwa wa aina yake uwanjani.

"Niliporudi hapa, nakumbuka mwandishi wa habari kwenye mkutano na waandishi wa habari alisema kwamba, kwa kawaida wale wanaorudi walikokuwa wanaweza kufanya vibaya zaidi," alisema Ibrahimovic akiiambia DAZN baada ya ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Sassuolo, Jumapili.

"Nilimjibu kwamba nitapambana ili kuinua klabu na kushinda taji la Scudetto. Hakuna aliyeamini, lakini tuko hapa, tumefanya kazi kwa bidii na kujitolea sana."

Ibrahimovic alikuwa mchezaji mkuu wa Milan waliposhinda taji la Serie A msimu wa 2010-11, baada ya hapo awali kuwa kinara wa Juve na Inter. Tangu wakati huo amezichezea Paris Saint-Germain, Manchester United na LA Galaxy.

Alitambua juhudi zake za uchezaji mwaka huu zimekuwa na ushawishi mdogo kuliko katika kampeni mbili zilizopita, na mkataba wake unatarajiwa kumalizika mwezi ujao.

"Lakini nadhani nimekuwa muhimu kwa kundi hili nje ya uwanja," aliongeza.

Milan walikusanya pointi 86 kwenye Serie A msimu huu na kushinda taji hilo. Akimzungumzia Raiola, Ibrahimovic alisema: "Nalitoa taji hili kwa Mino Raiola. Hili ni taji la kwanza kutwaa bila yeye.

"Niliporudi Ulaya, nilikuwa karibu na Napoli, kisha nikamuuliza ni wapi naweza kwenda kuleta mabadiliko na akajibu kuwa mimi pekee ndiye ninaweza kuikoa Milan."

Akizungumzia kuhusu kuendelea kucheza alisema: "Nina imani naweza kucheza msimu mwingine, haijalishi umri nilionao. Kama nitakuwa fiti nitaendelea kucheza na kucheza tena."

Ibrahimovic alivuta sigara na kusherehekea kwa shampeni baada ya Milan kubeba Scudetto.

LIVE IN PLAY
CHEZA USHINDE JACKPOT
TZS. 222,

MECHI KALI
RUVU SHOOTING
VERSUS
AZAM
1 | 3.11
X | 2.87
2 | 2.32

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# BAYERN WAONYWA KUHUSU LEWANDOWSKI KUTUA BARCA




**MUNICH,** Ujerumani

BAYERN Munich ni "historia" kwa Robert Lewandowski huku wakati huo akitaka kutimiza "ndoto" ya kuhamia Barcelona, kwa mujibu wa wakala wa mshambuliaji huyo, Pini Zahavi.

Maswali yamebaki kuhusu mustakabali wa Lewandowski baada ya kusema anataka kuondoka Bayern na amekataa kusaini mkataba mpya.


Lewandowski alisema hakuna lolote jipya kwenye ofa ya mkataba mpya aliyopewa, huku mkataba wake wa sasa ukimalizika mwishoni mwa msimu huu na mabingwa hao wa Bundesliga.

Hata hivyo, Mtendaji Mkuu wa Bayern, Oliver Kahn alisisitiza Jumamosi kwamba "ofa halisi" ilikuwa mezani, huku Mkurugenzi wa Michezo, Hasan Salihamidzic akimshutumu Zahavi kwa kujaribu kumgeuza kichwa mteja wake.

Zahavi alimjibu Salihamidzic huku akiwaonya Bayern kuwa halitakuwa jambo la busara kukataa kumwachia Lewandowski kwa uhamisho wa bure, wala kumnyima fursa ya kujiunga na Barca ya Xavi.

"Kwa Lewandowski, Bayern ni historia," Zahavi alliambia BILD.

"Robert ana nafasi ya kuhamia klabu ambayo amekuwa akiitamani siku zote. Kwa nini Bayern inamnyima nafasi hii?




## Klopp awapongeza Guardiola, Cit

**LONDON,** England

JURGEN Klopp alitoa pongezi zake kwa Pep Guardiola na Manchester City baada ya kutoka nyuma na kuwafunga Aston Villa na kutwaa taji la Ligi Kuu England siku ya mwisho ya msimu wa 2021/22, juzi.

City walikuwa wamefungwa na Villa mabao 2-0 baada ya dakika 70, lakini mabao matatu katika kipindi cha pili ndani ya dakika sita yalibadilisha mambo na kupata taji la ligi.

Liverpool waliwafunga Wolves mabao 3-1 kwenye Uwanja wa Anfield, ingawa hawakuweza kuwazuia City kushinda taji lao la nne ndani ya miaka mitano.

'Wekundu' hao bado wako mbioni kushinda taji la tatu msimu huu, wakiwa tayari wametwaa Kombe la EFL na FA, huku fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Real Madrid ikiwasubiri Jumamosi. Man City walishinda ligi taji hilo kwa kufikisha pointi 93, huku Liverpoool wakimaliza na pointi 92 katika mbio hizo za ubingwa.

"Hongera Man City na
Pep Guardiola. Asante
Aston Villa na Wolverha
ton kwa kufanya mch
mzuri," alisema Klopp
iambia Sky Sports baada
mchezo huo.

"Sio matokeo tuliyot
Ulikuwa ni mchezo wa
pindua matokeo. Sijui
tokeo haswa, lakini na
(Villa) walikuwa mbele
bao 1-0 - walikuwa m
kwa mabao 2-0 pia?

"Huwezi kufanya zaid
kutoa ubora wako kabisa
ndivyo vijana walivyofa
Tuliikimbiza timu bora z
duniani."

## HABARI MICHEZO

.883,040

# JACKPOT
## MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 25/05/22 | 13:00 | Vegalta Sendai vs Fagiano Okayama | 2.52 | 3.11 | 2.62 |
| 02. 25/05/22 | 13:00 | V Varen Nagasaki vs JEF United Chiba | 2.38 | 2.76 | 3.15 |
| 03. 25/05/22 | 13:00 | Thespakusatsu vs Roasso Kumamoto | 2.62 | 2.96 | 2.62 |
| 04. 25/05/22 | 13:00 | Shimizu S Pulse vs FC Tokyo | 2.59 | 3.13 | 2.54 |
| 05. 25/05/22 | 13:00 | Cerezo Osaka vs Urawa Red Diamonds | 2.76 | 3.10 | 2.40 |
| 06. 25/05/22 | 13:30 | Ventforet Kofu vs Tokushima Vortis | 2.43 | 2.81 | 3.01 |
| 07. 25/05/22 | 19:00 | Kristiansund vs Tromso | 2.75 | 3.40 | 2.40 |
| 08. 25/05/22 | 22:00 | Roma vs Feyenoord | 2.29 | 3.35 | 3.00 |
| 09. 26/05/22 | 05:30 | LA Galaxy vs Los Angeles FC | 2.36 | 3.59 | 2.52 |
| 10. 26/05/22 | 20:00 | AJ Auxerre vs St Etienne | 2.47 | 3.14 | 2.84 |
| 11. 26/05/22 | 20:45 | Kayserispor vs Sivasspor | 2.58 | 3.16 | 2.53 |
| 12. 26/05/22 | 21:00 | Sarpsborg vs Molde | 2.46 | 3.47 | 2.63 |
| 13. 26/05/22 | 21:00 | Vitesse Arnhem vs AZ Alkmaar | 2.87 | 3.37 | 2.30 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### JUMANNE - 24/05/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:00 | 2648 | Mbeya City vs Coastal Union | 2.14 | 2.85 | 4.00 |
| 14:00 | 5721 | Gokulam Kerala FC vs Bashundhara Kings | 2.02 | 3.31 | 3.31 |
| 15:15 | 3448 | Kuching FA vs Terengganu FC 2 | 2.63 | 3.16 | 2.48 |
| 15:30 | 4854 | Bayburt Idare vs Bodrumspor | 2.13 | 3.12 | 3.22 |
| 16:00 | 5736 | Ruvu Shooting vs Azam | 3.11 | 2.87 | 2.32 |
| 17:00 | 3289 | Club Guarani De Trinidad vs Fernando Mora | 2.63 | 2.88 | 2.68 |
| 17:00 | 4196 | Bunyodkor vs Nasaf Qarshi | 3.46 | 3.27 | 1.98 |
| 17:00 | 4742 | Sogdiyona Jizzax vs Kokand 1912 | 1.76 | 3.16 | 4.66 |
| 17:30 | 5081 | FK Auda vs FK Liepaja | 3.50 | 3.26 | 1.97 |
| 18:00 | 4293 | Kuressaare vs Nomme Kalju | 6.61 | 4.47 | 1.38 |
| 18:30 | 1860 | Aluminium Arak vs Peykan FC | 2.33 | 2.44 | 3.85 |
| 18:30 | 2406 | Teraktor Sazi vs Fajr Sepasi | 2.33 | 2.48 | 3.75 |
| 18:30 | 2624 | MES Rafsanjan vs Esteghlal Tehran | 3.56 | 2.58 | 2.32 |
| 18:30 | 2723 | Zob Ahan vs Nassaji Mazandaran | 2.06 | 2.58 | 4.38 |
| 18:30 | 2768 | Persepolis FC vs Padideh Mashhad | 1.24 | 5.20 | 14.00 |
| 18:30 | 2994 | Foolad Khuzestan vs Sepahan Esfahan | 3.79 | 2.41 | 2.37 |
| 18:30 | 4491 | Naft Masjed Soleyman FC vs Sanat Naft Abadan | 2.35 | 2.54 | 3.56 |
| 18:30 | 5199 | Havadar vs Gol Gohar | 3.22 | 2.40 | 2.68 |
| 18:30 | 5706 | FK Tukums 2000/Tss vs Valmiera Fk/Bjss | 21.47 | 9.56 | 1.05 |
| 19:00 | 1883 | MSK Zilina vs AS Trencin | 2.06 | 3.60 | 2.97 |
| 19:00 | 4233 | Atalanta Youth vs Juventus Youth | 2.12 | 3.74 | 2.77 |
| 19:15 | 2552 | Al Salmiyah vs Kazma SC | 2.40 | 3.39 | 2.57 |
| 19:30 | 3965 | Enppi Club vs Ghazl EL Mahallah | 2.59 | 2.64 | 3.23 |
| 19:30 | 4784 | Tiller IL vs Byaasen Toppfotball | 7.00 | 5.83 | 1.27 |
| 20:00 | 2023 | Tarsus vs Bursa Niluferspor | 1.87 | 3.17 | 4.00 |
| 20:00 | 2669 | Ostersunds vs Orgryte IS | 3.02 | 3.43 | 2.29 |
| 20:00 | 2799 | Jonkopings Sodra vs Skovde Aik | 2.15 | 3.58 | 3.18 |
| 20:00 | 3594 | Paide Linnameeskond vs Tammeka Tartu | 1.32 | 4.78 | 7.61 |
| 20:30 | 1709 | Hapoel Beer Sheva vs Maccabi Haifa | 3.27 | 3.03 | 2.16 |
| 20:30 | 2248 | Dunajska Streda vs Liptovsky Mikulas | 1.45 | 4.28 | 5.65 |
| 20:30 | 4996 | Orlando Pirates vs Maritzburg Utd | 1.85 | 3.02 | 4.76 |
| 21:00 | 1917 | Estudiantes de La Plata vs Atletico Lanus W | 2.36 | 3.65 | 2.70 |
| 21:00 | 2094 | CD Villa Espanola vs CA Cerro | 3.50 | 2.96 | 2.10 |
| 21:00 | 3733 | SBV Excelsior vs ADO Den Haag | 1.95 | 3.82 | 3.27 |
| 21:00 | 5745 | Juventud LP vs CA Atenas De San Carlos | 2.34 | 2.86 | 3.10 |
| 21:30 | 1919 | Dynamo Dresden vs Kaiserslautern | 2.23 | 3.19 | 3.24 |
| 21:30 | 2374 | Villefranche Sur Saone vs US Quevilly Rouen | 2.11 | 3.07 | 3.57 |
| 21:35 | 3340 | Huracan vs Deportivo Madryn | 1.64 | 3.80 | 5.00 |
| 21:45 | 1813 | Halifax vs Chesterfield | 2.34 | 3.31 | 2.81 |
| 22:00 | 1509 | Strindheim IL vs Melhus | 1.35 | 5.23 | 6.01 |
| 22:00 | 2380 | Tenerife Sur W vs SC Huelva W | 1.49 | 4.17 | 5.24 |
| 22:15 | 4765 | Breidablik Kopavogur W vs Valur Reykjavik W | 2.52 | 3.74 | 2.29 |

### JUMATANO - 25/05/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01:15 | 3170 | Santos vs Banfield | 1.26 | 4.66 | 10.69 |
| 01:30 | 5585 | Sp. San Lorenzo vs Independiente Fbc | 3.12 | 3.02 | 2.23 |
| 03:30 | 1841 | Flamengo vs Sporting Cristal | 1.09 | 7.77 | 19.42 |
| 03:30 | 2945 | Palmeiras vs Deportivo Tachira | 1.11 | 7.04 | 16.61 |
| 03:30 | 3787 | Ponte Preta vs Chapecoense | 2.25 | 2.92 | 3.21 |
| 03:30 | 5410 | LDU Quito vs Atletico GO | 1.68 | 3.50 | 4.57 |
| 03:30 | 5986 | Defensa Justicia vs Antofagasta | 1.37 | 4.57 | 6.61 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# SERENGETI GIRLS HAIJAMALIZA KAZI KWA CAMEROON - SHIME

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa timu ya Taifa ya Wanawake ya Tanzania chini ya umri wa miaka 17 (Serengeti Girls), Bakari Shime, amesema bado wana kazi kubwa ya kujipanga kwa mbinu tofauti kwa ajili ya mechi ya marudiano dhidi ya Cameroon, kuwania kufuzu Kombe la Dunia.

**Kikosi cha Serengeti Girls, juzi kilifanikiwa kuibuka ushindi wa mabao 4-1 ugenini dhidi ya Cameroon katika mchezo wa kwanza uliopigwa Uwanja wa Ahmadou Ahidjo jijini Yaounde.**

Serengeti Girls itakuwa mwenyeji katika Uwanja wa Amaan, Visiwani Zanzibar kwenye mchezo marudiano, ambao sasa itakuwa ikihitaji sare yoyote au kutoruhusu kufungwa zaidi ya mabao 2-0, ili kukata tiketi kushiriki Fainali za Kombe la Dunia kwa wasichana chini ya umri wa miaka 17, mwaka huu nchini India.

Akizungumza na gazeti hili jana, Shime aliwapongeza wachezaji wake kwa kupambana na kujitolea kwa hali na mali katika kuhakikisha wamefanya kile ambacho amekifundisha katika mazoezi na kukihamishia uwanjani kwenye mchezo huo.

Alisema ushindi wa juzi ni moja ya msingi mzuri kwa mchezo wao wa marudiano kwa sababu wanahitaji kujiandaa kimbinu na kiufundi kuhakikisha wanapata matokeo mazuri katika mchezo wa marudiano.

"Nawapongeza wachezaji wangu wamefanya kile nilichowapa mazoezi na ushindi huo kwetu ni msingi mzuri na furaha hii si ya muda mrefu kwa sababu tuna kibarua kingine katika mchezo wetu wa marudiano dhidi ya Cameroon, tutakaocheza nyumbani," alisema Shime.

Katibu Mkuu wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Wilfred Kidao, pia amewapongeza wachezaji hao kwa kupambana na kuibuka na ushindi kwa sababu mechi ilikuwa ngumu na ya ushindani mkubwa.

Alisema baada ya mechi hiyo wachezaji wanarejea kambini kujiandaa na mchezo wa marudiano kuhakikisha wanaendeleza walipoishia kwa kutafuta matokeo katika mchezo wa marudiano.

"Mechi bado haijaisha, tunaenda kumaliza kazi nyumbani, tunatakiwa kujipanga mara mbili zaidi kiufundi na kuwajenga kisaikolojia na akili wachezaji wetu kwa sababu mchezo huo ni fainali kwetu," alisema Kidao.




Mchezaji wa Gofu, Angel Eaton (katikati), akikabidhiwa kikombe na Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Dk. Stergomena Lawrence Tax (kushoto), baada ya kutangazwa mshindi kwenye shindano la wanawake (Lugalo Ladies Open 2022), lililomalizika mwishoni mwa wiki, Lugalo, Dar es Salaam. Kulia ni Meneja wa Kampuni ya Ndege ya Qatar nchini Tanzania, Anil Sreenivasan. **NA MPIGAPICHA WETU**

# *Stergomena aipongeza timu ya Gofu Wanawake*

**Na Saada Akida**

WAZIRI wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Dk. Stergomena Lawrence Tax, amesema kuna mengi ya kujivunia kwa timu ya Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania ya Gofu ya Wanawake (TPDF Lugalo Golf Club) yakiwamo ya kuitangaza Tanzania ndani na nje ya nchi.

Kauli hiyo alitoa juzi katika ufungaji wa mashindano ya 'Lugalo Ladies Open 2022' yaliyofanyika siku mbili, Jumamosi na Jumapili katika viwanja vya klabu hiyo vilivyopo Kawe, Dar es Salaam.

Mashindano hayo yalishirikisha klabu sita za wanawake ambazo ni Dar es Salaam Gymkhana, Arusha, Kilimanjaro, TPC, Morogoro na wachezaji wawili kutoka Uganda.

Akizungumza na gazeti hili jana, Stergomena alisema timu hiyo imeendelea kufanya vizuri kwa kuibuka washindi inapocheza na timu za ndani na hata zile za nje ya nchi.

"Yapo mengi ya kujivunia katika klabu hii, hasa Timu ya Gofu ya Wanawake, kweli inaitangaza Tanzania ndani na nje ya nchi na hasa inapocheza nje ya nchi," alisema.

Alisema timu hiyo ilishinda ilivyocheza na nchi za Nigeria, Ghana, Kenya na Uganda, pia imeweza kutoa mchango mkubwa kwa timu ya taifa.

"Wito wangu kwa kampuni, taasisi na wadau mbalimbali wa michezo, ni kuchangia harambee ili timu ya Wanawake ya Lugalo ijiandae vizuri, pia kuongeza uwezo katika mazoezi yao, ninachangia Sh. milioni 25 katika harambee hii," alisema.

Naye Mwenyekiti wa Klabu ya Lugalo, Brigedia Jenerali Mstaafu, Michael Luwongo, alisema klabu hiyo inaongoza kwa idadi kubwa wachezaji wanawake.

Alisema mashindano hayo yamepangwa na kuratibiwa na wanawake wenyewe kwa ajili ya kuleta ushindani.

# Michezo

Jumanne Mei 24, 2022
Nipashe



Bayern waonywa kuhusu Lewandowski UKURASA 22

MILIKI...



Winga wa Yanga, Faridi Mussa, akimiliki mpira dhidi ya safu ya ulinzi ya Biashara United kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza jana na kumalizika kwa sare ya bao 1-1. **MPIGAPICHA WETU**

# *Yanga bado pointi 3 bingwa*

## Biashara yaigomea kubakiza alama moja, Mayele, Mpole ni vita...

**Na Adam Fungamwango**

BAO la Mkenya Collin Opare, katika dakika ya 77, liliinyima Yanga nafasi ya kubakiza pointi moja kutangazwa bingwa wa Ligi Kuu Bara msimu wa 2021/22 baada ya timu hizo kutoka sare ya 1-1 kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza jana.

**Straika Mkongomani Fiston Mayele, anayekimbizana na George Mpole wa Geita Gold FC kwenye mbio za kuwania Kiatu cha Dhahabu Ligi Kuu Bara, aliitanguliza Yanga kupata bao la kuongoza dakika ya 74 kabla ya wenyeji hao kuchomoa dakika tatu baadaye kupitia kwa Opare.**

Kwa bao hilo, sasa Mayele ana mabao 14 sawa na Mpole ambaye juzi alitimiza idadi hiyo wakati wakitoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Mabingwa Watetezi, Simba uwanjani hapo.

Vinara hao wa Ligi Kuu walikuwa wanahitaji pointi tatu kubakiza moja tu ili waweze kutangazwa kuwa mabingwa kwa msimu wa 2021/22, lakini walipunguzwa kasi na sasa wanahitaji ushindi kwenye mechi inayofuata dhidi ya Coastal Union Juni 8, mwaka huu katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Iwapo itapata ushindi kwenye mechi hiyo, itafikisha pointi 67, ambazo Simba yenye pointi 51 haiwezi kuzifikia kwani hata kama ikishinda mechi zote tano ilizobakisha itafikisha alama 66 tu.

Kwenye mechi ya jana ambayo hadi mapumziko hakukuwa na lolote, mabao yote mawili yalifungwa dakika 16 za mwisho kabla mechi kumalizika.

Mayele alifunga bao hilo baada ya kupokea mpira mrefu wa Saido Ntibazonkiza ulimsababisha mfungaji kukimbizana na mabeki wawili wa Biashara United ambao hawakuwa na la kufanya zaidi ya kumsindikiza, hali iliyosababisha kipa kutoka golini.

Wakati akitoka, Mayele aliudokoa kwa juu, ukampita kipa huyo na kujaa wavuni kuhesabu bao la kwanza kwenye mechi hiyo.

Bao hilo lilidumu kwa dakika tatu kabla ya Opare kupachika la kusawazisha akiunganisha krosi iliyochongwa na Mkenya mwenzake, Ambrose Awio.

Mechi ilianza kwa Chico Ushindi kuikosesha Yanga bao dakika ya 10 tu ya mchezo, baada ya kumegewa pande na Faridi Mussa, dakika tatu baadaye, Fiston Mayele alipiga krosi safi ambayo Feisal Salum alitakiwa kuugusa mpira utumbukie ndani ya nyavu, lakini alikosa.

Mfululizo wa Yanga kukosa mabao uliendelea, Dickson Ambundo naye ilikuwa zamu yake dakika ya 23, alipomegewa pasi ya kisigino na Mayele, akiwa ndani ya eneo la hatari alipiga shuti kubwa akapaisha mpira juu.

Shambulizi pekee la Biashara United kipindi cha kwanza lilikuwa dakika ya 30 wakati Atupele Green alipopewa pande na Ramadhani Chombo 'Redondo', kwa mshangao wa wengi, akiwa yeye na kipa Aboutwalib Mshery, si tu kwamba alipiga shuti kubwa juu, lakini pembeni kabisa ya lango.

Chico, raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo aliupata mpira akiwa nje kidogo ya eneo la hatari, akamlamba chenga nahodha wa Biashara United Abdulmajid Mangalo na kuingia ndani, lakini shuti lake lilishindwa kulenga lango na kutoka nje.

Timu zote zilifanya mabadiliko kipindi cha pili Yanga ikiwatoa Dickson Ambundo, Ushindi, Farid Mussa na Yassin Mustapha, ikiwaingiza Denis Nkane, Ntibazonkiza, Jesus Moloko na Heritier Makambo, huku Biashara United ikiwaingiza Benson Magige, Shaaban Ada ambaye naye baadaye alitoka, kuchukua nafasi za Atupele, Cristin Zigah, huku Tabo Donald akiingia nafasi ya Ada.

Ni mabadiliko ambayo yaliifanya mechi hiyo kuwa ya wazi zaidi na kushambuliana kwa zamu hadi kupatikana kwa mabao hayo. Yanga sasa imefikisha pointi 64 kileleni wakati Biashara imefikisha pointi 24, ikiwa nafasi ya 14.

## Pablo sasa asikitishwa na uchezaji Simba

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Simba, Pablo Franco, ameonekana kuisikitikia timu yake ya Simba na kusema wachezaji wake wanaonekana kushindwa kabisa kupambana inapocheza na timu za katikati au juu ya msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, akisema ni jambo lisilopendeza kwa klabu kubwa kama hiyo.

Wakati akiongea hayo, Kocha Mkuu wa Geita Gold, Fred Felix Minziro, amelalamikia umakini kwa wachezaji wa Kitanzania, akidai kama wangekuwa makini kidogo, basi mechi ya juzi dhidi ya Simba kwenye Uwanja wa CCM Kirumba timu yake ingeondoka na ushindi na wala isingekuwa sare ya bao 1-1.

Makocha wote wawili waliongea hayo baada ya kumalizika kwa mechi hiyo ya raundi ya 25 ya Ligi Kuu Tanzania Bara huku Pablo akionekana kukikatia tamaa kabisa kikosi chake akisema anafikiri sasa kimedhohofika kabisa kimwili na kiakili.

"Uhalisia ni kwamba hatuchezi vizuri tunapokuwa ugenini, sina ninachoweza kubadilisha kwa jambo hilo. Kiwango cha wachezaji wangu kilikuwa chini sana, siyo kiungo tu pekee, ila timu nzima, mistari yote, kuzuia, kushambulia, na hata mipira ya kutenga, nafikiri kwa sasa tumedhohofika kabisa kimwili, na kiakili, leo (juzi) hatukuwa sawa kabisa na hatukuwa na tamaa ya ushindi ukilinganisha na mechi zilizopita," alisema kocha huyo raia wa Hispania na kuongeza.

"Baada ya dakika 60 tulisambaratika kabisa, tuko kwenye wakati mgumu, mara kwa mara tunakabiliwa na majeruhi na hicho ndicho kiwango chetu cha sasa, kila tunapokabiliana na timu za katikati na juu ya msimamo tumeshindwa kabisa kupambana, bila shaka haitoshi kwa klabu kubwa kama Simba," alilalama Pablo.

Naye Minziro aliwalalamikia wachezaji wake kutokuwa makini kwani waliikamata mechi na hawakustahili kutoka sare.

"Nikiri tumepambana na timu kubwa na zuri, ila umakini kwa wachezaji wetu wa Kitanzania bado, wachezaji wangu wangekuwa makini wangeweza kufunga mabao mawili au matatu mwishoni mwa mchezo. Walishindwa kumalizia mipira, tungekuwa makini hii mechi ya leo (juzi) isingekuwa sare, tungeshinda," alisema Minziro.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >